SportPesa
TZS. 918,137,180
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mfumo kuondoa watoto mitaani sasa waja rasmi**

UKURASA 3



**HAALAND SASA ATAJWA KUMRITHI MBAPPE PSG**

UKURASA 21


# Nipashe

Alhamisi Februari 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580852

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Samia: Nasikia sauti ya Magufuli



• **Asema** kila anapozindua miradi inamkumbusha mambo aliyoyaasisi...

*Uk. 2*



# Shahidi kesi Mbowe augua kizimbani, kesi yaahirishwa

UK. 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MABULA ATAJA KIPAUMBELE BAADA YA KIAPO**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ametaja kipaumbele cha wizara kuwa ni kuanza na ukaguzi na kuyatambua maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji...

UKURASA WA 4

**MBARONI AKIDAIWA KUTAKA KUMHONGA WAZIRI**

MAMLAKA ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), inamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Eden kwa tuhuma za kutaka kutoa rushwa kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ...

UKURASA WA 4

**RIPOTI YA CAG YAWAWEKA MATATANI**

VIGOGO watano wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, wamesimamishwa...


**Tahadhari maambukizi UVIKO - 19 D' Salaam**

UKURASA 3


**MICHEZO** PABLO AISHTUKIA ASEC, AISOMA, AIONYA SIMBA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan pamoja Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinumwi Adesina (kushoto), wakifungua pazia kuweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje ya Km 112.3, katika eneo la Veyula, jijini Dodoma jana, itakayotoka Ihumwa – Matumbulu – Nala -Veyula - Ihumwa. **PICHA: IKULU**

# Shughuli za kibinadamu tishio Bwawa la Nyerere

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

BUNGE limeishauri serikali kuchukua hatua za haraka kunusuru bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoharibu mazingira kwenye Bonde la Mto Kilombero, zikitishia upatikanaji wa maji. Vilevile, uharibifu huo unatishia mradi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo itategemea umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere. Chombo hicho cha kutunga sheria pia kimeshauri kupandisha hadhi Bonde la Mto Kilombero kuwa Hifadhi ya Taifa ili kulitumia Jeshi la Uhifadhi kulinda na kuelimisha jamii pamoja na kuwaondoa wananchi wote wanaofanya shughuli za kijamii kwenye eneo hilo. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Ally Makoa, akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo bungeni jana, alisema kero zinazolikabili Bonde la Kilombero ni kubwa na zinatakiwa kushughulikiwa kwa jicho la pekee.

Alisema bonde hilo limebainika kuwa linakabiliwa na kero za matumizi mabaya ya ardhi ya bonde kama vile uvamizi wa shughuli za kibinadamu zisizo endelevu kama vile uvuvi, kilimo, ufugaji na uanzishwaji wa makazi holela.

"Hali hiyo imeathiri kwa kiwango kikubwa uhifadhi wa bonde na kutishia kupoteza sifa ya kuendelea kuwa moja ya maeneo manne yaliyotambuliwa kama yenye ardhi oevu, kupungua kwa mtiririko wa maji kuelekea Bwawa la Nyerere na hivyo kutishia uendelevu wa mradi wa kufua umeme na mradi wa SGR unaotegemea umeme kutoka bwawa hilo," alihadharisha.

Makoa pia alisema kunachangia kutoweka au kupungua kwa bioanuai za wanyamapori, misitu na samaki.

"Bunge linaishauri serikali kutekeleza mambo yafuatayo; kulinda mazingira yasiendelee kuharibiwa na shughuli za kijamii na kiuchumi zinazoendelea, kuimarisha ulinzi wa bonde kwa kutumia Jeshi la Uhifadhi pamoja na kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi wa bonde na kuwaelimisha wananchi wanaozunguka hifadhi ya bonde kuhusu umuhimu wa kulinda na kulihifadhi bonde.

# Shahidi kesi ya Mbowe augua kizimbani, kesi yaahirishwa

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 13 wa Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu, Inspekta Tumaini Swila, amezidiwa akiwa kizimbani, akidai hajisikii vizuri, hivyo kuomba kesi iahirishwe kwa madai kwamba hawezi kuendelea kuhojiwa.

Hayo yalitokea jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Joachim Tiganga, wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala.

Shahidi alihojiwa kuanzia saa 4:00 asubuhi, lakini ilipofika saa 7:45 mchana, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, aliomba kesi iahirishwe kwa madai kuwa shahidi kapata tatizo ghafla.

"Mheshimiwa Jaji, shahidi hajisikii vizuri kabisa na kapata tatizo ghafla. Tunaomba shauri liahirishwe hadi kesho tuone itakuwaje baada ya kupata matibabu," alidai Kidando. Wakili Kibatala alipinga akidai shauri hilo linaahirishwa kwa sababu nyingine na si sababu ya ugonjwa.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja hizo ilikubali kuahirisha shauri hilo hadi leo saa 3:00 asubuhi.

Kabla ya kuugua, katika ushahidi wake, Swila alidai wakati washtakiwa Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya wanakutana na Luteni Dennis Urio, Mbowe alikuwa hawajui.

Shahidi alidai hafahamu kama baba yake Ling'wenya baada ya mwanawe kuchukuliwa na Urio aliitisha kikao cha familia kujadili suala hilo.

Inspekta Swila alidai wakati Urio anazungumza na Mbowe hakuwapo lakini si lazima kupima maneno ya Mbowe na Urio bali yafanyiwe kazi maneno ya Urio.

Shahidi alidai kuwa hakuwahi kwenda Cassa Motel ambako Mbowe alikutana na Urio na kwamba hakuwahi kwenda Kikosi cha 92 KJ Ngerengere kuchunguza kama Urio alikuwa bado yuko kazini. Alidai kuwa hafahamu kikosi hicho na wala hafahamu kama Luteni Urio baada ya kurejea kutoka Darfur alikamatwa kikosini baada ya kutajwa na Kasekwa.

Shahidi huyo alidai kuwa ukitumia fedha kwa ajili ya kufadhili ugaidi ikaenda kutumika kwa kilimo utakuwa umefadhili ugaidi.

Alidai Mbowe alimtumia Luteni Urio Sh. 500,000 kwa ajili ya kufadhili vitendo vya ugaidi, kulipua vituo vya mafuta, kukata miti barabarani na kuwadhuru viongozi wa serikali.

Hata hivyo, alidai kuwa hafahamu kama Luteni Urio alitoa Sh. 300,000 katika Sh. 500,000 anazodai kutumiwa na Mbowe, akawapa Lijenje na Bwire.

Akisoma maelezo ya mshtakiwa wa pili, Kasekwa, alidai kuwa alilipwa Sh. 87,000 na Luteni Urio.

Wakili Kidando alipinga shahidi kuhojiwa kwa kutumia maelezo ya Luteni Urio lakini Wakili Kibatala alipinga akidai maombi ya kupinga yasikubaliwe kwa kuwa wanataka kuficha ushahidi.

Hata hivyo, mahakama ilikubali maelezo hayo yaendelee kutumika kwa ajili ya shahidi kuhojiwa maswali kwa sababu ni mpelelezi katika kesi hiyo.

Baada ya kuruhusu maelezo hayo yatumike, muda mfupi upande wa Jamhuri kupitia Wakili Kidando waliomba kesi iahirishwe kwa madai ya shahidi hajisikii vizuri kabisa.

Shahidi wakati anapanda kizimbani asubuhi alidai mahakamani kwamba hayuko vizuri, alianza kujisikia vibaya tangu juzi jioni lakini ataendelea kutoa ushahidi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Mbowe ambao wanashtakiwa kwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

# Samia: Nasikia sauti ya Magufuli

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kila anaposhiriki matukio ya uzinduzi wa miradi mbalimbali, amekuwa akisikia sauti ya Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli, ikimkumbusha juu ya miradi aliyoiasisi.

Mkuu wa nchi alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje ya jiji hilo yenye urefu wa kilomita 112.3.

"Mwenzenu siku kama ya leo toka asubuhi huwa nasikia sauti ya mtangulizi wangu, Dk. John Pombe Magufuli ananiambia kuhusu miradi hii, kuhusu Dodoma kuwa makao makuu, kuhusu mambo mengi na leo hii tunasimama hapa kuweka jiwe la msingi la mradi huu.

"Lakini kazi hii Waswahili wanasema 'ukiona vyaelea ujue vimeundwa'. Kwa bahati nzuri muundaji wa suala hili aliyetekeleza maono ya Baba wa Taifa kuhamia Dodoma akataka kuipanga Dodoma.

"Mungu amemchukua mapema, lakini aliniachia urithi mzito na niliahidi mawazo yote aliyoyaanzisha nakwenda kuyatekeleza kikamilifu," Rais Samia alisema.

Alibainisha kuwa uwekaji wa jiwe hilo la msingi ni moja kati ya utekelezaji wa mawazo aliyoyaanzisha Hayati Rais Magufuli.

"Nami niwaahidi kwa kuungwa mkono vyema na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na wadau wengine tunakwenda kukamilisha mradi huu wa ujenzi wa barabara ya mzunguko kama alivyotaka ufanywe," alisisitiza.

Rais Samia alisema kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo kutasaidia kuufungua Mkoa wa Dodoma pamoja na kuiunganisha Tanzania na mataifa mengine.

"Barabara hii inakwenda kuturahisishia Tanzania kufanya biashara na Afrika kwa nchi zingine kuja Tanzania na sisi kwenda maeneo mengine ya Afrika," alisema.

Rais Samia alisema mradi huo utakapokamilika utakuwa kichocheo kikuu cha kukuza uzalishaji na usafirishaji kwenda kwenye masoko ya bidhaa za mazao ya kilimo pamoja na zile za viwandani ili kukuza uchumi wa nchi.

"Ni mategemeo yangu barabara hii wizara husika kupitia TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania), makandarasi pamoja na wasimamizi wote kwa pamoja mtasimamia kuhakikisha mradi huu ukamilike kwa wakati uliopangwa ili kutoa fursa ya maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," aliagiza.

Rais pia aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya barabara kwa kuwa serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha kuitekeleza.

"Ujenzi wa kilomita moja ya barabara kwa sasa ni kama Sh. bilioni 1.2 hadi bilioni 1.5, hivyo wananchi mnapaswa kulinda miundombinu ya barabara kwa kuacha kung'oa vibao vya alama za barabarani pamoja na kubomoa," alisema.

Rais wa AfDB, Dk. Akinwumi Adesina, alisema wataendelea kushirikiana na Tanzania katika kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema anampongeza Rais Samia kwa kuendelea miradi ambayo mtangulizi wake Hayati Magufuli alikuwa ameiasisi.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema lengo la mradi huo ni kuondoa msongamano wa magari katika Jiji la Dodoma.

Alisema mradi huo wa ujenzi wa barabara za mzunguko utatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka benki hiyo na Serikali ya Tanzania.

"Barabara hii ya mzunguko ipo kilomita 20 kutoka katikati ya Jiji la Dodoma yenye urefu wa kilomita 112.3 ambayo ujenzi wake utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 249.339," alibainisha.

# Mfumo kuondoa watoto mitaani waja

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imetangaza kuanzisha mfumo maalumu utakaowezesha kuondoa watoto wa mitaani na kuagiza walioko nyumbani kwa wazazi wao ama walezi kubakia huko.

Kadhalika, serikali imesema inaandaa mpango utakaokomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini.

Akizungumza jana jijini Mwanza katika uzinduzi wa kituo maalumu cha malezi na makuzi katika soko la Mirongo wilayani Nyamagana, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Doroth Gwajima, alisema mfumo huo utasaidia kumaliza tatizo la watoto wa mitaani.

Alisema kuna sababu nyingi zinazochangia watoto wa mitaani ikiwamo ukatili wanaofanyiwa na walezi ama wazazi wao pamoja na umaskini wa kipato katika familia.

Aliongeza kuwa kupitia mfumo huo, serikali itahakikisha watoto wote wanaishi majumbani badala ya kukaa mitaani na kuishi katika maisha magumu.

Alitaja sababu zinginze zinazochangia kuwapo watoto wa mitaani ni vitendo vya ndugu kudhulumu mali za wajane, hali inayosababisha mama kushindwa kuwatunza.

Akizungumzia mpango wa kukabiliana na tatizo la ukatili wa kijinsia, alisema serikali itaziwezesha familia za watoto wa mitaani ili zijimudu kwa kipato.

Alisema familia nyingi zinashindwa kutunza na kuwalea watoto wao kutokana na kuwa na kipato kidogo, hali inayosababisha kukimbilia mijini kuomba mitaani.

Aliongeza kuwa wizara yake inalinda makundi yote ya kijamii wakiwamo watoto, wanawake, wenye ulemavu pamoja na wanaume ili kuhakikisha wote wanakuwa na maisha mazuri na kuishi salama.

Akizungumza katika uzinduzi katika kituo cha malezi na makuzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kutetea Haki za Wanawake na Watoto la Kivulini, Yasin Ally, alisema, wameanza kupambana na ukatili wa kijinsia kwa kuwasaidia wanawake wanaofanya biashara katika masoko.

Aliongeza kuwa sehemu za masoko ni miongoni mwa maeneo yenye ukatili wa kijinsia, na kwamba wameanzia huko kwa kutoa elimu, kujengea mazingira bora ya kufanyia biashara na wengine kuwapatia mitaji.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Tusonge, Debora Mahanga (katikati), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa Msimamizi wa Watoto wanaolelewa katika Kituo cha watoto yatima cha Msongola, Christina Charles, wakati taasisi hiyo kwa kushirikiana na uongozi na wanafunzi wa Shule ya Zawadi ya Mwembeni Kivule, walipotembelea kituo hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dar yatakiwa hadhari kasi maambukizi ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

WADAU wameshauri wakazi wa mkoani Dar es Salaam kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya ikiwamo kupata chanjo, ili kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19.

Ushauri wao unatokana na taarifa iliyotolewa juzi na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, kuwa mkoa huo unaongoza kwa idadi kubwa ya watu waliothibitika kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa UVIKO-19, kwa kuwa na wagonjwa wapya 184 kati ya visa vipya 252 vilivyoripotiwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, alisema, bila wananchi kuchukua tahadhari, ugonjwa huo unaweza kuendelea kujikita mkoani humo.

"Kwanza kabisa, Dar es Salaam ina mwingiliano mkubwa wa watu kutoka ndani na nje ya nchi, lakini watu hawachukui tahadhari na kwa mtindo huo wa maisha, unaweza kusababisha kuwapo kwa tatizo hilo, kwani wengi hawana muda wa kuchukua tahadhari," alisema Mawinza.

Alisema, serikali inaelekeza kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kutojazana kwenye vyombo vya usafiri, kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka, na kwamba kwa sasa watu wengi hawazingatii hayo.

"Usafiri mwingi kwa wakazi wa Dar es Salaam ni ule wa umma, lakini watu hawachukui tahadhari, ninadhani ipo haja ya kuongeza kasi ya kuelimisha jamii na ikiwezekana hata kwa shuruti, kwani ugonjwa upo," alisema.

Alisema, wao kama WAJIKI wana waelimishaji rika ambao wamekuwa wakipita nyumba kwa nyumba katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke na kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, jijini Dar es Salaam kilichoko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Seleman Bishagazi, alisema sababu kubwa ya mkoa huo kuongoza kwa vifaa vipya vya UVIKO-19 ni dharau.

"Mkoa wa Dar es Salaam unaweza kuwa unaongoza kwa watu wake kuwa na dharau dhidi ya corona, kwani wanauchukulia ugonjwa huo kama jambo la kawaida, hali hiyo inachangia katika maambukizi," alisema Bishagazi.

Alisema, njia ambayo itasaidia kupunguza kasi ya maambukizi, ni kuwawezesha waelimishaji ngazi ya jamii ili wawe wanapita hata nyumba kwa nyumba kuhimiza umuhimu wa kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya. "Waelimishaji ngazi ya jamii wapo, lakini hawana jukwaa la kuwawezesha kufanya kazi hiyo. Ni vyema wakawezeshwa kama ilivyo kwa wengine wakiwamo wa vikundi vya VICOBA," alisema.

Katika taarifa yake, Mganga Mkuu alisema, visa vipya ni kati ya watu 8,529 waliopimwa katika kipindi hicho, sawa na asilimia tatu, na kwamba visa hivyo vimeripotiwa katika kipindi cha Januari 29 hadi Februari 6, mwaka huu, huku wagonjwa wapya 76 kati ya 78 waliolazwa wakiwa ni wale ambao hawajachanjwa na vifo vilikuwa vitatu.

Kwamba, tangu ugonjwa huu uliporipotiwa kwa mara ya kwanza nchini Machi 2020 hadi kufikia Februari 6, mwaka huu,, jumla ya watu 33,482 walithibitika ( sawa na asilimia 7.6) kati ya 442,566 waliopima na jumla ya watu 792 wamepoteza maisha.

Alifafanua kuwa, kwa siku ya Februari 6, mwaka huu, wagonjwa mahututi tisa waliripotiwa na wote walikuwa ambao hawajachanja chanjo ya UVIKO-19 na mgonjwa mmoja ameripotiwa kuwa kwenye mashine ya kusaidia kupumua na alikuwa hajachanjwa.

Mganga huyo alisema vifo vitatu vilivyotokea kwa kipindi hicho katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Manyara vyote vilikuwa vya wagonjwa ambao hawajachanjwa.

Aidha, alisema, tangu kuanza kwa zoezi la uchanjaji nchini mwaka jana, hadi kufikia Februari 6, mwaka huu jumla ya watu 2,117,387 (sawa na asilimia 3.67) wamepata dozi kamili ya chanjo.

# Mabula ataja kipaumbele baada ya kuapishwa

**Munir Shemweta na Magreth Lyimo,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema wizara yake itaanza ukaguzi na kuyatambua maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji nchini.

Dk. Mabula alisema hayo jana jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kuapishwa na Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo.

"Maeneo haya lazima tuyafanyie ukaguzi pamoja na kuyatambua hasa yale ya vijijini ambayo ardhi yake inahitaji uhaulishaji ili kupunguza muda wa mwekezaji kusubiri pale anapohitaji ardhi ya kufanya uwekezaji," alisema.

"Vipaumbele vya wizara haviwezi kwenda tofauti na vipaumbele vya Rais ambapo ameelekeza suala zima la uwekezaji. Sisi wizara tutafanya ukaguzi wa maeneo yote yaliyotengwa tuyatambue na tujue wenzetu wa TIC, TAMISEMI, EPZA ardhi waliyo nayo ni kiasi gani na wamepanga kufanya nini," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri, halmashauri kwa maana ya TAMISEMI kupitia mipango kabambe katika maeneo yao kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na wizara itahitaji kujua kiasi gani cha maeneo yaliyoko yamepangwa kwa makusudio gani.

Alisema lengo la wizara ni kutwaa maeneo hayo kuwa chini ya serikali ili mwekezaji atakapofika serikali iweze kumpeleka kwa kuwa kutakuwa na kanzidata ya maeneo husika.

"Kwenye maeneo ya vijiji, kuna maeneo mengi ambayo yana fursa nzuri za uwekezaji ambapo ardhi ya vijiji inasimamiwa na Sheria Na. 5 ili kumilikiwa inabidi uhaulishaji katika maeneo yaliyokusudiwa kuwa ya uwekezaji ufanyike kwa ukamilifu na kuwe na umiliki wa eneo ili mwekezaji atakapokuja tusianze kufanya mikutano ya wananchi ili wakubali," alisema Dk. Mabula.

Kuhusu migogoro ya ardhi, Dk. Mabula alisema migogoro ya ardhi inagusa wizara tano za kisekta na inatokea kwa sababu hapajawekewa mpango wa matumizi ya ardhi kwa nchi nzima na kubainisha kuwa, wizara itazungumza na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa maana ya halmashauri zote ili kuona kwa jinsi gani patakuwa na jambo la makusudi kabisa la kuhakikisha kwamba walau vijiji na maeneo mengi yanapangiwa matumizi ya ardhi.


## MOPEH COMPANY LIMITED

Box 590, Mob.,+255 0785 335544 , 0713 639979, 0673 335528, P. O. Box 32372 Dar es Salaam – TANZANIA
Mob. +255 (0)785335544, +255(0)673335528, +255(0)755731072,
Email: info@mopeh.co.tz, mopehltd20@gmail.com Web: www.mopeh.co.tz

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK** tunatoa muda wa siku 14 kwa mdaiwa aliyeorodheshwa kwenye jedwali hapa chini awe amelipa deni analodaiwa na benki pamoja na gharama za Kampuni, kunyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali iliyowekwa kama dhamana ya mkopo aliokopa kwa mujibu wa mkataba husika. Mnada utafanyika sehemu mali ilipo, siku na tarehe kama itakavyotangazwa kwenye vipeperushi na gari la matangazo.

| TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 23 FEB 2022 | 10;30 ASUBUHI | NKANYANGA COMPANY LIMITED | NYUMBA | GONGO LA MBO-ILALA |
| 23 FEB 2022 | 15;00 ALASIRI | KIVAULA M LUHANGA | NYUMBA | GONGO LA MBOTO - ILALA |
| 23 FEB 2022 | 11.00AM ASUBUHI | PASTORI MWASHUKA TEMBA | NYUMBA | GONGO LA MBOTO-ILALA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa malipo ya asilimia 25% ya fedha taslim papo hapo baada ya nyundo ya dalali, na ndani ya siku 14 toka siku mnada mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 75% ya salio.
2. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo na sehemu ilipo.
3. Mnunuzi atakaposhindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.
4. Mali / dhamana zitauzwa kama zilivyo.
5. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba zilizohapo juu au nenda tawi lolote la Letshego Bank lililo karibu nawe.

116697802

# Raia Korea mbaroni madai kutaka kumhonga waziri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), inamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Eden kwa tuhuma za kutaka kutoa rushwa kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Makarani Ahmed, alimtaja mtuhumiwa huyo ni Kang Juem Suek (66), raia wa Korea Kusini.

Alisema Februari 8, mwaka huu, saa tano asubuhi, mtuhumiwa huyo alikamatwa kwa kosa la kumshawishi na kutoa rushwa ya Dola za Marekani 1,300 kwa Waziri Simai.

Makarani alisema mtuhumiwa huyo alitoa rushwa hiyo kwa lengo la kutaka kurudishiwa shule yake iliyoko Shakani Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ambayo ilifutiwa usajili na wizara.

Alisema ZAECA inaendelea kumuhoji mtuhumiwa huyo na uchunguzi utakapokamilika, atafikishwa katika vyombo vingine vya sheria.

Shule hiyo ilifutiwa usajili mwaka jana kutoendelea kutoa elimu kutokana na kukiuka taratibu na sheria ikiwamo kukiuka taratibu za uwekezaji na kushindwa kulipa kodi.

Licha ya shule hiyo kufutiwa usajili, lakini iliibuka kuwa kinara kati ya shule 10 zilizofanya vizuri katika mitihani ya darasa la sita, matokeo ambayo yalitolewa mwaka huu na Wizara ya Elimu.




Makamu wa Rais wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), Victorious Kamuntu, akifungua mafunzo yaliyowashirikisha wadau mbalimbali kuhusu taratibu na sheria za kusajili makampuni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mfumo kidijitali kuboresha makazi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imekamilisha uandaaji ramani za kidijitali zinazotumika kama ramani za msingi kwenye utekelezaji mfumo wa anwani za makazi katika halmashauri 38 nchini.

Aidha, wataalamu wa wizara wanaendelea kutekeleza kazi ya kubadilisha ramani kutoka kwenye mfumo wa analogia kwenda dijitali na kutambua maeneo yasiyopimwa na kuandaa ramani za mipaka ya kiutawala katika halmashauri.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, wakati wa uzinduzi wa operesheni maalumu ya kukamilisha uwekaji anwani za makazi uliofanyika ukumbi wa mkutano wa Jakaya Kikwete Convention Centre, Dodoma.

Kwa mujibu wa Ridhiwani, wizara imejipanga kikamilifu kuhakikisha uandaaji wa ramani za kidijitali unakamilika ndani ya muda ili kuwezesha utoaji anwani za makazi.

"Wizara tutanufaika sana na taarifa zinazokusanywa kwenye mfumo wa anwani za makazi kutokana na kutumia taarifa hizo kuhakikisha tunaboresha taarifa zilizopo kwenye mifumo ya usimamizi wa ardhi, kuimarisha ukusanyaji mapato ya ardhi na kuboresha utoaji huduma za ardhi kwa kutumia anuani za makazi.

Naibu Waziri aliongeza kuwa kazi hiyo ya kubadilisha ramani kutoka mfumo wa analogia kwenda digitali, ilianza katika halmashauri zote tano za mkoa wa Dar es Salaam, jiji la Dodoma na halmashauri zingine za mikoa ya Tabora, Kagera, Tanga na Mbeya.

"Iwapo jambo hili litafanyika kikamilifu nchi nzima, litawezesha wizara kuongeza uwezo wa kusimamia uendelezaji miji, utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia ya kidijitali kwa kuwa ramani zote za mipango miji na upimaji zitakuwa kwenye mfumo huo zikibainisha viwanja au mashamba na matumizi yake," alisema.

Ridhiwani alisema ulinganifu wa kitakwimu utawezesha wizara kutoa huduma bora zaidi na kusimamia upatikanaji taarifa za wamiliki wa ardhi kupitia mfumo unganishi wa taarifa za ardhi (ILMIS). Pia alisema utarahisisha kutambua maeneo kwa ajili ya uwekezaji, na shughuli mbalimbali kama makazi mashamba na maeneo ya kufugia na shughuli za uchumi.

Mbali na faida za kitakwimu zinazopatikana kwenye anwani za makazi, alibainisha kuwa lengo la uandaaji ramani hizo ni kurahisisha upatikanaji taarifa sahihi za ardhi ambazo ni muhimu katika kujenga msingi wa anwani za makazi pamoja na utekelezaji maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha ardhi inapangwa, inapimwa na kurasmishwa.

# Ripoti ya CAG yawaweka matatani vigogo h/shauri

**Na Abdallah Khamis,**
MTWARA

VIGOGO watano wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, mkoani Mtwara, wamesimamishwa kazi kutokana na ripoti maalumu ya ukaguzi iliyofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kati ya Mei 24 hadi Julai 3, mwaka jana.

Mbali na watumishi hao watano kusimamishwa kazi, wengine wawili wamepewa onyo kali kufuatia ripoti hiyo.

Waliosimamishwa kazi ni Mweka Hazina, Heri Hamad; Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji, Abdillah Mfinanga; Mtendaji wa Kata ya Mkuti, Jamadi Saidi; Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mbonde, Mariam Madaga na Ofisa Manunuzi, Hasina Marumbwe.

Waliopewa onyo ni fundi mitambo, Leonard Gondole na Mhasibu Chambu Samuel.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkurugenzi wa Mji wa Masasi, Elias Ntiruhungwa, alisema watumishi hao saba ni miongoni mwa watumishi 14 waliotajwa katika ripoti hiyo.

Alisema watumishi hao wamehusishwa katika tuhuma mbalimbali ikiwamo matumizi mabaya ya ofisi, ubadhirifu wa fedha na kukiuka kanuni, taratibu na sheria za utumishi wa umma "Halmashauri tulifanya kikao kujadili ripoti ya ukaguzi maalumu ambao ulifanyika kuanzia Mei 24 hadi Julai 3, 2021, baada ya kuipokea ripoti hiyo tuliipitia na baadaye kuipeleka kwenye kamati ya fedha," alisema Ntiruhungwa.

Alisema baada ya kupitia mapendekezo ya taarifa hiyo waliona kuna haja ya kuchukua hatua katika yale yaliyokuwa katika mamlaka ya ofisi yake, lakini alisema hana mamlaka ya kuwataja wengine waliohusika kwenye ripoti hiyo, kwa kuwa hawapo katika mamlaka ya Halmashauri ya Masasi.

"Watumishi wote ambao ripoti hiyo imewataja kuhusika kwa njia moja au nyingine wanahusishwa kukiuka taratibu na sheria mbalimbali za serikali zikiwamo Sheria ya Fedha, Sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria Ndogo za Halmashauri, Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 na marekebisho yake."

Aliongeza kuwa kwenye uchambuzi wa ripoti waligundua watumishi 14 wanatakiwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na walipoenda katika utekelezaji walikuta watumishi saba ndio ambao mpaka sasa wanatakiwa kuchukuliwa hatua za nidhamu na mamlaka ya kinidhamu ambayo ni Halmashauri ya Mji wa Masasi, kwa kuwa wengine wameshaondoka katika halmashauri hiyo.

Ntiruhungwa aliongeza kuwa wameshapeleka barua kwa Katibu Mkuu TAMISEMI kwa ajili ya ushauri wa namna bora ya kuwawajibisha watumishi waliokuwa nje ya mamlaka ya Halmashauri ya Masasi Mji.

Alisema kwa sasa watumishi saba walioko katika halmashauri hiyo wameshapewa barua ya kujieleza ndani ya siku 14 na majibu yao ndiyo yatakayoamua kuona adhabu gani ya kuwatia hatiani.

Aliwataja sita wasiokuwa katika mamlaka ya nidhamu ya halmashauri hiyo ni, Salim Samuel, aliyehamishiwa Nanyumbu, Masoud Mwinjuma (Jiji la Dodoma), Sospeter Makene (Mwanza), Mwajabu Mkinda, (Korogwe TC), Bwire Chibule (Tandahimba) na Charles Kapule (Simiyu).

Hata hivyo, hakumtaja mtumishi wa saba aliyehamishwa huku Mwenyekiti wa Halmashauri ya mji huo, Hashim Namtumba, akisema ni aliyekuwa Mkurugenzi wao, Gimbana Ntavyo, aliyehamishiwa Halmashauri ya Mji wa Tarime, mkoani Mara.

# TANGAZO

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 197 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

SWAHILI CERAMIC STORE……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Managing Director
Swahili Ceramic Store
Plot No. 54, Chang'ombe Road, Temeke Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17th day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 26th day of JAN 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 195 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

TAUSI ARNOLD MUSHI……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Tausi Arnold Mushi
Mwnani Village, Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17TH day of FEBRUARY 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25TH day of JANUARY 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 181 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

BERNARD KIREI……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Bernard Kirei,
Plot No. 2037, Block A, Tip Top Street, Manzese Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17 day of 02 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25 day of 01 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 189 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

KHALFAN HEMED KHALFAN……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Khalfan Hemed Khalfan
Plot No. 586, Block B, Mbezi Area
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 16 day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27th day of January 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dar chukueni hatua UVIKO-19 bado ipo

**TAARIFA** iliyotolewa juzi na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, inaonyesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa idadi kubwa zaidi ya watu waliothibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19.

Kwamba, mkoa huo una wagonjwa wapya 184 kati ya visa vipya 252 vilivyoripotiwa, ambavyo vimeripotiwa katika kipindi cha Januari 29 hadi Februari 6, mwaka huu, huku wagonjwa wapya 76 kati ya 78 walilazwa wakiwa ni ambao hawajachanjwa na vifo vilikuwa vitatu.

Mganga huyo anafafanua kuwa tangu ugonjwa huo ulivyoripotiwa kwa mara ya kwanza nchini Machi 2020 hadi kufikia Februari 6, mwaka huu, jumla ya watu 33,482 walithibitika kuugua sawa na asilimia 7.6 kati ya 442,566 waliopima na jumla ya watu 792 wamepoteza maisha.

Kutokana na takwimu hizo, Wizara ya Afya inawataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zote zinazoelekezwa kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, ikiwamo kuchanja chanjo ya UVIKO-19.

Lakini pia anasema serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo nchini, ili kuwezesha wananchi kupata kinga ya ugonjwa huo, na kwamba hadi Februari 6, mwaka huu, dozi 9,845,774 za chanjo zilikuwa zimepokewa nchini.

Kwa mujibu wa Mganga huyo Mkuu, tangu kuanza kwa zoezi la uchanjaji nchini mpaka kufikia Februari 6, mwaka huu jumla ya watu 2,117,387, sawa na asilimia 3.67 wamepata dozi kamili ya chanjo.

Pamoja na hayo, anawataka wananchi kuhakikisha wanapata dozi kamili za chanjo, kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kuvaa barakoa kwa usahihi, kuzingatia usafi binafsi kwa kunawa mikono, kuwahi kwenye vituo vya afya wanapohisi dalili za ugonjwa huo na kuzingatia kufanya mazoezi.

Kimsingi, taarifa hiyo imeweka wazi ukweli halisi kuhusu ukubwa wa tatizo la ugonjwa huo nchini kwa takwimu za Mkoa wa Dar es Salaam, ambao unachukuliwa kuwa na idadi kubwa ya watu.

Kutokana na hali hiyo, nasi tunadhani kwamba si wakati wa kuendelea kupuuza kuhusu uwapo wa ugonjwa huo na athari zake, hivyo wakazi wa Dar waache kulala bali kila mmoja achukue tahadhari zote zinazotakiwa kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, kwani ni wazi kwamba wakazi wengi hawafuati maelekezo.

Mitaani mikusanyiko inaendelea kama kawaida, ndani ya usafiri wa umma hasa daladala abiria wanajazana kama kawaida, karibu wote hawavai barakoa kana kwamba ugonjwa huo haupo nchini.

Katika mazingira hayo, tunaona kuna haja ya kuwakumbusha wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuzingatia maelekezo yote yanayohusu kujikinga na ugonjwa huo hatari ikiwamo kujitokeza kupata chanjo yake inayotolewa bure.

Ikumbukwe, Mganga Mkuu anasema, visa vimeripotiwa katika kipindi cha Januari 29 hadi Februari 6, mwaka huu, huku wagonjwa wapya 76 kati ya 78 waliolazwa wakiwa ni wale ambao hawajachanjwa na vifo vikiwa ni vitatu.


Hapo tushauri kwamba, hali hiyo inatosha kuamsha wananchi kuwa makini kwa kuchukua tahadhari zote, ikiwamo kujitokeza kwa wingi kwenda katika vituo vilivyotengwa kwa ajili ya kutolea chanjo ya UVIKO-19.

Takwimu hizi zinapaswa kuwazindua Watanzania kwamba kupata chanjo ya UVIKO-19 ndiyo njia sahihi na salama kwa maisha yao kwa kuwa zimethibitisha kuwa wanaokaidi kuchanja ndio wanaokufa na kupata maambukizi.

Tunaona mkazo unaosisitizwa, ni wananchi wajitokeze kupata dozi kamili za chanjo, kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kuvaa barakoa kwa usahihi, kuzingatia usafi binafsi kwa kunawa mikono, kuwahi kwenye vituo vya afya wanapohisi dalili za ugonjwa huo na kuzingatia kufanya mazoezi.

Tangu mwishoni mwa Julai mwaka jana, chanjo ilipozinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan, inaelezwa kuwa ni watu 2,117,387, sawa na asilimia 3.67 ambao wamepata dozi kamili ya chanjo. Kwa takwimu hizi ni wazi kuna kusuasua katika kujitokeza kupata chanjo, na ikumbukwe kuwa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla siyo kisiwa kisichofikika, hivyo wananchi wajitokeze kuchanja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Jenifer Gilla

## Muungwana Lazima Nilonge

# Sera mpya mazingira, iwe chachu kupambania mabadiliko tabianchi

**FEBRUARI** 12 au keshokutwa, ni siku muhimu kitaifa katika muktadha wa mazingira, kwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.

Sera hiyo imejumuisha masuala ya mazingira yaliyokuwamo katika sera ya mwaka 1977 na kuongeza mapya sita, ambayo ni udhibiti wa taka za kielektroniki; uchafuzi katika shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi; usimamizi wa matumizi ya kemikali; mabadiliko ya tabianchi; kudhibiti viumbe hai; na usimamizi wa matumizi salama ya baioteknolojia ya kisasa.

Ni uzinduzi unaoambatana na shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira hadi siku ya kilele hicho, kuanzia tarehe kama hiyo mwaka jana. Hapo ni sehemu ya kuonyesha masuala ya msingi yanayoelekezwa katika sera mpya, ikiwamo kupanda miti na kusafisha mazingira.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mary Maganga, anafafanua kuwa sera hiyo inaongeza wigo inakoshughulikia na changamoto za mazingira zinazopaswa kufanyiwa kazi katika kipindi husika, ili kuleta maendeleo endelevu.

Serikali inapaswa kupongezwa kwa uamuzi wa kuibadilisha sera hiyo na kuongeza maeneo muhimu, ikiwamo suala la mabadiliko ya tabianchi, kwa kuwa ndio adui mkuu wa mazingira na kikwazo za maendeleo endelevu.

Kuwapo kipengele cha mabadiliko ya tabianchi katika sera mpya, kunaonyesha namna serikali imedhamiria kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoisumbua dunia kwa sasa.

Athari zinaoneka wazi kwa sasa, ikiwamo mvua isiyotabirika na ama kwa kiwango kikubwa au kidogo, tofauti na matarajio yaliyokoo.

Ni hali inayosababisha athari nyingi, moja kubwa ni shughuli za kilimo ama kusimama au kuyumba katika baadhi ya mikoa.

Mabadiliko ya tabianchi yanachangia kuwapo joto kali na linalovuka kiwango stahiki, kutokana na tabaka la juu la dunia (ozone layer) kuwa wazi na kuruhusu miale ya jua kupita moja kwa moja hadi duniani. Hapo inachangia kuwapo ukame, mazao kukauka kabla hayajakomaa na maradhi kwa viumbe hai.

Ni matumaini kuwa sera hiyo mpya itakuwa mwongozo kwa jamii, wa namna ya kupambana na athari ili utekelezaji wake uwe unaoleta tija kwa taifa kwa muktadha wa utunzaji wa mazingira yetu.

Shime wanajamii, tufuate maelekezo yanayotolewa kupitia sera hiyo na vyombo vya umma na wakala mamlaka binafsi katika kuhakikisha mazingira yetu tunayalinda na kuyatunza. Kama sera inataka kila mwananchi apande walau miti mitatu katika nyumba yake,basi na iwe hivyo.

Sote basi tufanye hivyo bila ya kusukumwa, kwa kuwa upo usemi 'Tunza mazingira nayo yakutunze'. Kwa serikali na wadau wa mazingira, ni wajibu wao wahakikishe wanasimamia miongozo iliyoko katika sera.

Hiyo ni msaada kupambana na changamoto mpya za kimazingira zinazoendelea kujitokeza, kutokana na mabadiliko ya mifumo kiuchumi, kijamii na kimazingira yanayoendelea duniani.

Walimu nao wapewe sura ya mtaala unaofundisha miongozo hiyo kwa wanafunzi, ili ufundishaji wao uwajengee watoto ari ya kutunza mazingira na kuona umuhimu wa mazingira bora tangu umri mdogo na kurejesha uasilia uliokuwapo kabla ya kuharibika, kutokana na shughuli za kibinadamu.

Ripoti zinaonyesha nchi zenye kiwango kikubwa cha uchafuzi wa hali ya hewa, ziko hatarini zaidi kuwa na viwango vikubwa vya magonjwa yasioyakuambukizwa na kuchangia asilimia 72 ya vifo vyote, asilimia 16 katika vifo hivyo vinachangiwa na sumu inayotokana na uchafuzi wa hali ya hewa.

# TANGAZO

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 177 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

ABDULRAHMAN MOHAMOUD DALMAR..............................ACCUSED PERSON

To:
Abdulrahman Mohamoud Dalmar
Plot No. 277, Block A, Bagamoni Area
Ilala Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 16 day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of January 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name..............................

Signature..............................

Qualification/Relationship
Date..............................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 205 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

HUSSEIN ATHUMAN FUNDI..............................1ST ACCUSED PERSON
SALLY ATHUMAN FUNDI..............................2ND ACCUSED PERSON

To:
Hussein Athuman Fundi & Sally Athuman Fundi
Plot No. 2013, Block A, Kijitonyama Area
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17th day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of JAN. 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name..............................

Signature..............................

Qualification/Relationship
Date..............................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 192 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

GIBORE GWESO NYAMBEGA..............................ACCUSED PERSON

To:
Gibore Gweso Nyambega
Kijichi Area, Kigamboni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17th day of February 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of January 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name..............................

Signature..............................

Qualification/Relationship
Date..............................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 184 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

KABAZA GELASIUS RUNYETA..............................ACCUSED PERSON

To:
Kabaza Gelasius Runyeta
Plot No.1266 & 1267, Mbweni Area
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17 day of FEB 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 28 day of JAN 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name..............................

Signature..............................

Qualification/Relationship
Date..............................



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (kushoto) na Mkurugenzi wa Kampuni ya GF Trucks Equipment's Ltd, Imran Karmali, wakitiliana saini mkataba, jijini Dodoma jana, wa kusambaza vifaa kwa ajili ya miradi ya maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge waunga huduma mkono kwa mkono

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

UMOJA wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), wamesema wanaunga jitihada za huduma ya mkono kwa mkono, wakiomba isambae nchi zima ili kusaidia waathirika wa matukio ya ukatili wa jinsia.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa TWPG, Shally Raymond, wakati wa kikao kazi cha viongozi wa umoja huo jana bungeni, huku wataalamu kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Polisi, Hospitali na Maofisa Ustawi wa Jamii wakieleza hali halisi ya ukatili wilayani Kinondoni.

Kikao hicho kilijumuisha wabunge wanaume ambao ni vinara wa ukatili wa kijinsia na eneo la mfano la Kinondoni, ambalo kwa mujibu wa wataalamu hao linaongoza kwa ukatili.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema kwa zaidi ya miezi mitatu kumekuwa na matukio ya mauaji ambayo chanzo cha awali kimeelezwa ni mahusiano, na ndiyo maana wakaja na mradi wa huduma ya mkono kwa mkono ambao unaanzia Wilaya ya Kinondoni inayoongoza kwa matukio ya ukatili.

Naye Mratibu wa Kituo cha Mkono kwa Mkono manusura wa ukatili wa kijinsia Hospitali ya Mkoa wa Manyara, Asia Mkini, akiwasilisha mada kuhusu vituo hivyo, alisema huduma hiyo ni vituo vilivyoanzishwa mahususi kwa ajili ya kusaidia manusura wa ukatili wa kijinsia wapate huduma ndani ya jengo moja.

"Ndani ya kituo kuna huduma za ustawi wa jamii, kipolisi na kitabibu, huduma za kisheria kwa ajili ya kuwawezesha kupata tiba, vipimo, msaada wa kisaikolojia na kufungua kesi kwa usiri," alisema.

"Lengo la kuwa na vituo hivi ni kufanikiwa kutoa huduma kwa kuhakikisha kuwa manusura katika huduma anazopatiwa kwa kuwazingatia utu wake na heshima, kuwa na usiri wakati wa kupata huduma ili wasipate madhara," alisema Mkini.

Alisema hadi sasa kuna vituo 14 nchini huku changamoto kubwa ikiwa ni upatikanaji wa fedha na watumishi, na kuiomba serikali kufanyiakazi muda wote.

Ofisa Mwandamizi wa Polisi Wilaya ya Kinondoni, Christopher Neutron, alisema maeneo hayo huwa na askari maalum ambao hushughulikia kwa haraka kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa mahakamani.

Naye Wakili wa LHRC, Gatrude Gyabene, alisema wanatoa msaada wa kisheria kwa watu wote na katika utafiti walibaini:

"Wanaume wengi wana kesi za ardhi na migogoro kazini inaonyesha wako kwenye rasilimali, wanamiliki au kutaka kumiliki mali, lakini wanawake ni talaka, ndoa na mirathi."


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA

**TAARIFA KWA UMMA**

10 Februari, 2022

**KUHUISHA TAARIFA ZA MAJENGO YA BIASHARA YALIYOSAJILIWA NA TMDA**

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inapenda kuwajulisha wafanyabiashara wote wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi waliosajiliwa na TMDA kuhuisha taarifa za majengo yao pamoja na vibali vya kufanya biashara hadi ifikapo tarehe 30 Juni 2022.
2. Ili kufanikisha zoezi hilo, wafanyabiashara wote wanatakiwa kufika katika ofisi za kanda za TMDA na kuwasiliana na Mameneja husika kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana.
3. Aidha, kwa wale ambao waliwasilisha maombi ya usajili wa majengo kwa njia ya kielektroniki (online submission) watatakiwa kuingia katika tovuti ya TMDA www.tmda.go.tz na kuchagua E-services kisha bonyeza online premises (https://imis2.tmda.go.tz/portal/#/public/app-home) ili kuingia katika mfumo wa TMDA wa wateja (RIMS customer self service portal) na kuhuisha taarifa zao.
4. Tunapenda kuwafahamisha wateja wetu kuwa kushindwa kufanya uhuishaji wa taarifa za majengo yao kutasababisha majengo hayo kufutwa katika orodha ya majengo yaliyosajiliwa na TMDA.
5. Hatua ambayo itasababisha pale wanapohitaji kuendelea na biashara, kutakiwa kusajili upya majengo hayo.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**
**S. L. P 1253, Dodoma**
**S. L. P 77150, Dar Es Salaam**
**Simu: +255 222450512/ 2450751/ 2452108**
**Simu bila Malipo: 0800110084**
**Barua pepe: info@tmda.go.tz**
**Tovuti: www.tmda.go.tz**

216698802


# Ubadhirifu mikopo wamng'oa ofisa maendeleo

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, amemtaka Mkurugezi wa Manispaa ya Temeke, kumsimamisha Ofisa wa maendeleo ya jamii kutokana na kutaka kumhamisha mtumishi aliyefichua udanganyifu katika utoaji wa mikopo.

Alitoa maelekezo hayo jana alipokuwa akipokea taarifa ya kamati aliyoiunda kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Pia Jokate alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Elihuruma Mabelya, kwa kukataa kuuza shule kwa Sh. milioni 100.

Alisema udanganyifu si maono ya Rais kwa kuwa kulikuwa na ukakasi katika utoaji wa mikopo jambo lililosababisha kuunda kamati ya uchunguzi. Alisisitiza kuwa wale wote wanaosimama katika haki na wanaosaidia viongozi kutimiza majukumu yao kwa kusimamia haki ni lazima walindwe.

"Hatuwezi kutetea wale ambao wanasababisha kasoro na tukawaacha wale ambao wanatusaidia kazi. Chini ya uongozi wangu, sitaruhusu hilo na inawezekena hili lisiwapendeze sana lakini sidhani kwamba tuko kwenye hizi kazi kufurahishana. Mwisho wa siku nitakuja kuulizwa mimi kama mkuu wa wilaya kwamba hili limetokea wewe ulikuwa wapi na ulichukua hatua zipi.

"Sasa nilisema na ninaendelea kusema kila mtu ashike hamsini zake. Kila mtu asimame kwenye wajibu wake. Uzalendo wako, uadilifu wako, mienendo yako ndiyo ikutetee kitu tunachokitaka na si vinginevyo. Tusibebeshane lawama ambazo hazistahili, tuwachukulie hatua wale wote wanaoenda kinyume cha taratibu. Lazima tuivushe wilaya yetu mahali pazuri zaidi," alisema.

Mwenyekiti wa kamati ya ufuatiliaji mikopo hiyo, Sadath Mtwale, akiwasilisha taarifa hiyo, alisema uchunguzi ulibaini kuwa kuna baadhi ya vikundi ambavyo vilipatiwa mikopo bila kutimiza masharti yaliyoainishwa na kwamba hilo limesababishwa na baadhi ya viongozi wanaoingiza siasa katika utoaji wa mikopo hiyo.

"Baadhi ya vikundi vilivyoomba mikopo havijapitishwa katika ngazi ya kata na vikao vya baraza la kata lakini vimepitishwa katika ngazi ya manispaa na kungojea kupewa mikopo. Pia baadhi ya vikundi havijafuata utaratibu wa uombaji wa mikopo kwani kuna ambavyo vinajaziwa fomu ya uombaji wa mikopo wakati bado havijasajiliwa.

"Baadhi ya vikundi vimetengenezwa kiujanja ujanja na miongoni mwa wajumbe wake wanatoka nje ya kata husika. Pia baadhi ya watendaji wa kata wakishirikiana na maofisa maendeleo wa kata wamekuwa na tabia ya kubadilisha muhtasari wa vikao vya baraza la kata ili kuongeza majina katika vikundi ambavyo vitapatiwa mikopo," alisema Mtware.

Alisema timu hiyo ilipitia vikundi 117 na kubaini vikundi 21 ambavyo baadhi ya wajumbe walishindwa kujitokeza mbele ya kamati na kwamba waliofika walishindwa kujibu maswali yanayohusu vikundi vyao na kuonyesha kutowajua wajumbe wenzao. Alisema hali waliyoitilia mashaka kuwa hawapo.

Pia alisema baadhi ya wanufaika ni viongozi wa manispaa hiyo ambao wamekuwa wakishiriki kutengeneza vikundi kwa ajili ya kupata mikopo kwa manufaa yao. Alisema baadhi ya fomu za utambulisho wa vikundi zimekuwa zikitiwa saini na watendaji na wenyeviti wa mitaa tofauti na ile ambayo vikundi vipo.

"Baadhi ya waheshimiwa wamekuwa wakiingilia utendaji wa vikundi wakilazimisha kufanyika uamuzi ambao wana maslahi nayo. Pia wamekuwa wakilazimisha kufukuzwa kwa baadhi ya wana vikundi kutokana na kuwa na misimamo ya kutokukubaliana nao.

"Baadhi ya watendaji na maofisa maendeleo wa kata wamekuwa wakipokea vitisho na mashinikizo kutoka kwa waheshimiwa au watendaji ngazi ya manispaa kutokana na misimamo yao ya kiutendaji katika utoaji wa mikopo kwa vikundi," alidai Mtware.

# TANGAZO

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 199 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

HAIKA SHAYO.......................................................................ACCUSED PERSON

To:
Haika Shayo
Mbweni Area, Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this Court on the 16TH day of FEBRUARY 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27TH day of JANUARY 2022.

..............................................
RESIDENT MAGESTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

**Served Upon Me/us:**

Name..............................................

Signature..............................................

Qualification/Relationship

Date..............................................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 186 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

LUSUBILO MWAKABIBI...........................................................ACCUSED PERSON

To:
Lusubilo Mwakabibi
Kijitonyama Area,
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this Court on the 17 day of FEB 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 28 day of JAN 20 22

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

**Served Upon Me/us:**

Name..............................................

Signature..............................................

Qualification/Relationship

Date..............................................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 180 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

GLORIA MWINGIRA...........................................................ACCUSED PERSON

To:
Gloria Mwingira,
Plot No. 45, Block G, Magomeni Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this Court on the 17th day of February 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27th day of JAN 20 22

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

**Served Upon Me/us:**

Name..............................................

Signature..............................................

Qualification/Relationship

Date..............................................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 179 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

ADATUS KAPES.......................................................................ACCUSED PERSON

To:
Adatus Kapes,
Plot No. 3, Block A, Mbezi Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this Court on the 16 day of March 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of January 20 22

..............................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

**Served Upon Me/us:**

Name..............................................

Signature..............................................

Qualification/Relationship

Date..............................................

# Hatua 5 zilizowezesha wahitimu ajira zatajwa

BUNGE limeelezwa hatua tano zilizochukuliwa na serikali kuwawezesha wahitimu wa vyuo vikuu wasio na ajira kuajiriwa au kujiajiri.

Ofisi ya Waziri Mkuu ilitaja hatua hizo bungeni jana katika majibu yake kwenye swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali inachukua hatua gani kuwawezesha kulipa mikopo yao wahitimu wa vyuo vikuu ambao hawana ajira.

Ofisi hiyo ikijibu swali hilo, ilisema kwa wanufaika wa mkopo ambao baada ya kumaliza vyuo wanachukua muda mrefu kupata ajira au kujiajiri, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuwawezesha kuajiriwa au kujiajiri.

Ilitaja hatua hizo ni kutoa mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu wa elimu ya juu nchini kupitia waajiri wa ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya wahitimu 6,624 wamepatiwa mafunzo ya uzoefu wa kazi na wahitimu 11,475 wamepatiwa mafunzo ya kushindania fursa za ajira katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

Pia ilisema kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, jumla ya Sh. bilioni 3.3 zimetolewa katika kipindi cha miaka mitano kwa ajili kuwapatia vijana mikopo nafuu wakiwamo wahitimu wa vyuo vikuu.

Kadhalika, ilisema kupitia mikopo inayotolewa na halmashauri ya asilimia 10, jumla ya Sh. bilioni 145.8 zimetolewa kwa ajili ya mikopo kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Ilitaja hatua nyingine ni kutoa mafunzo ya ujasiriamali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, hadi sasa programu hiyo imewafikia vijana 8,736 wa elimu ya juu nchi nzima.

Ilisema kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi kwa kuweka miundombinu mbalimbali ya kiuchumi kama vile ya nishati, uchukuzi na mawasiliano.

Awali ilifafanua kuwa jukumu mojawapo la msingi la serikali ni kuandaa mazingira wezeshi kuhakikisha Watanzania wanapata maarifa na ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri na kuajirika ili kukuza uchumi wa Taifa na vipato vyao.

Kutokana na msingi huo, ilisema serikali kupitia Bunge ilitunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu namba tisa ya Mwaka 2004 ambayo inawezesha kutoa mikopo au ruzuku kwa wanafunzi wahitaji waliokidhi vigezo.

Ilisema kwa mujibu wa sheria hiyo, wazazi au wadhamini wanatakiwa kuhakikisha mikopo inarejeshwa ili kunufaisha Watanzania wengine wanaohitaji.



Mbunge wa Handeni, Reuben Kwagilwa, akiuliza swali Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mlima Kilimanjaro kutangazwa zaidi

SERIKALI imelihakikishia Bunge kuwa itaendelea kubuni mikakati zaidi ya kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwa maslahi mapana ya nchi.

Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa kauli hiyo jana bungeni katika majibu yake kwenye swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Maleko.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kuanzisha makongamano ya kimataifa ili kukuza utalii wa Mlima Kilimanjaro.

Wizara hiyo ikijibu swali hilo, ilisema kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikiendelea kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Ilitaja mbinu hizo ni onyesho la Utalii la Kimataifa la Kilifair linalofanyika Mjini Moshi Mwezi Juni kila mwaka, Mbio za Kilimanjaro (Kilimanjaro Marathon) zinazofanyika mkoani Kilimanjaro mwezi Februari kila mwaka.

Pia ilisema kushiriki makongamano ya kimataifa ikiwamo WTM – London, ITB - Ujerumani, Fitur-Hispania na Expo - 2020 Dubai.

Kadhalika, ilisema kushiriki makongamano ya kimataifa yanayolenga kuimarisha uhifadhi na kutangaza utalii wa Mlima Kilimanjaro likiwamo kongamano la milima mirefu duniani (International Mountains Alliance - ITA).

Ilibainisha kuwa Mlima Kilimanjaro ni moja ya eneo la urithi wa dunia ambapo kupitia mikutano mbalimbali ya UNESCO mlima huo hutangazwa.

Wizara hiyo ilitaja mbinu nyingine ni kuwatumia watalii wanaofika Tanzania kama mabalozi wa kuutangaza Mlima Kilimanjaro na kuendelea kutumia matukio muhimu ya kitaifa kama sherehe za Uhuru kuhamasisha jamii kupanda Mlima Kilimanjaro.

Vile vile, alisema kuandaa na kushiriki katika onyesho la kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Regional Tourism Expo – EARTE 2021) lililofanyika jijini Arusha ili kutangaza vivutio vya utalii ikiwamo Mlima Kilimanjaro.




Habari zote na Augusta Njoji

# Uchafuzi wa Ziwa Victoria walalamikiwa

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Juliana Masaburi, ameitaka serikali idhibiti uchafuzi unaofanyika pembezoni mwa Ziwa Victoria ambao unapunguza samaki kuzaliana.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema uchafuzi huo unasababisha shughuli za uvuvi kudorora.

Katika Majibu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), uchafuzi wa mazingira unaofanyika pembezoni mwa Ziwa Victoria unatokana na shughuli za kibinadamu zisizozingatia hifadhi ya mazingira.

Ilisema shughuli hizo ni pamoja na utiririshaji wa majitaka kutoka katika maeneo ya makazi, utupaji wa taka ngumu kutoka majumbani na viwandani.

Kilimo kisicho endelevu kinachosababisha uchafuzi wa maji kutokana na kuongezeka kwa tabaki, matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu na mbolea za viwandani na uchimbaji wa madini usio endelevu.

Kutokana na hali hiyo, ilisema serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni, miongozo na mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya maziwa.

Aidha, ilisema serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) inafanyika kwa miradi ya maendeleo iliyoko na inayotarajiwa kufanyika pembezoni mwa Ziwa Victoria ili kuhakikisha udhibiti wa vyanzo vya uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria utokanao na shughuli za kibinadamu zinazohusisha miradi hiyo.

Vile vile, ilisema serikali imepiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa ikichangia uchafuzi pembezoni mwa Ziwa Victoria.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 10, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## LHRC, JICA WAINGIA UBIA VITA UKATILI KIJINSIA NA NGONO ZEMBE



Ukurasa 12

## SIMULIZI TATA ZA WATUMIAJI DAWA KULEVYA, SAFARI NGUMU KUZIACHA

KILELE WIKI YA UKOMA..

# Dk. Mollel: Tunalenga mwaka 2030 ugonjwa ubaki kuwa historia

**Na Yasmine Protace**

UGONJWA wa ukoma kimsingi unatajwa kuambukizwa kupitia njia ya hewa, visababishi vikuu vikiwa ni bakteria.

Baada ya maambukizo, kuna kipindi mgonjwa hasikii dalili zake. Inaweza kudumu miaka mitano hadi 20 bila ya dalili na pale zinapoonekana, zinagusa maeneo kadhaa kama vile mfumo wa upumuaji, ngozi au macho.

Wakati dalili zinapoanza kuonekana, mgonjwa hasikii tena baridi, joto na maumivu. Kwa hiyo, anashindwa kutambua kirahisi. Vidonda vinavyotokea haviumi, uchafu pamoja na bakteria hatari wanaingia mwilini, hata kufanya baadhi ama hawatibu au wanachelewa kutibiwa.

Ndiyo sababu kuna wakoma wanapoteza viungo. Kuna aina mbili zinazotambulika kutokana na idadi ya bakteria zilizopo zinazotofautishwa na kiasi cha alama zenye ganzi mwilini.

Maradhi hayo hutokea zaidi miongoni mwa jamii ya hali ya chini na kuna baadhi ya watu wanaushirikisha na imani ya kurogwa. Pia, kuna familia zimekuwa zikiwatenga wenye ukoma.

Hata hivyo, inaelezwa kitaalamu kuwa mtu anayewahi kutibiwa ukoma, daima ni ngumu kupata ulemavu wa kudumu. Nchini, serikali imekuwa ikitoa dawa bure za ukoma pamoja na elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Mtazamo unatajwa inawezekana baadhi ya jamii hawana taarifa na kusababisha watu kuugua ukoma wakipata ulemavu wa kudumu, kwa sababu tu hawakupata matibabu kwa haraka.

Hivyo, inafafanuliwa kwamba mtu anayejihisi kuwa na dalili za ugonjwa huo, anatakiwa kufika hospitali kwa wakati apatiwe matibabu, kwani kitaalamu, baada ya hatua hiyo wanarudi katika hali za kawaida, lakini kinyume chake ni kupata ulemavu wa kudumu.




Shamrashamra za Siku ya Ukoma nchini, Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, aliyembeba mtoto. **PICHA: YASMINE PROTACE**.

**NAIBU WAZIRI AFYA**

Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, anawataka wataalamu wa afya nchini kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa ukoma ili ifikapo mwaka 2030 ugonjwa huo uwe umetokomea nchini.

Akizungumza kwenye Siku ya Ukoma Duniani, iliyofanyika katika eneo la Sukamahela wilayani Manyoni, mkoani Singida, Dk. Mollel, anafafanua:

"Wataalamu wamefanya kazi nzuri sana ya kuwatambua wenye ukoma, lakini bado tuna kazi kubwa mbele yetu kwa sababu tunataka miaka tisa ijayo kabla ya mwaka 2030 Ukoma uwe historia ndani ya Tanzania.

"Ni lazima tushikamane, tusiishie kwenye kutunza utu wa watu wenye ukoma tu, lakini tuhakikishe hakuna mwingine anayekwenda kupata ukoma na hata kama yupo basi tuhakikishe tunamtambua mapema, ili tumsaidie asiweze kupata ulemavu."

Anaendelea: "Ni lazima tuutokomeze ukoma, dawa za kuponyesha ukoma tunazo na zinatolewa bila malipo, kiwango cha maambukizi mapya kimeshuka na kufikia chini ya asilimia tano, pia asilimia 90 ya wagonjwa wote wapya tunaowaibua ni wagonjwa walioambukizwa miaka mingi iliyopita."

Naibu Waziri anatoa angalizo la kibajeti kuhusu ukoma, kuwa huenda fedha zinaweza kuwa zinatumika kujadili ukoma, kufanya semina zake na kumjadili mgonjwa husika, kuliko kiasi kinachoelekezwa kumtibu mgonjwa wa ukoma

Hivyo anawataka wataalamu wa afya kubadilisha mikakati ya mapambano dhidi ya ukoma, kwa kuwafikia wagonjwa walipo na kutoa elimu zaidi kwa wananchi dhidi ya maradhi ya ukoma.

AFYA

MAISHA NI MTIHANI...

# Simulizi tata za watumiaji dawa kulevya, safari ngumu kuziacha

■ Aina kuu tatu, kila moja na vionjo vyake

**Na Devota Mwachang'a**

WANAPOTAJWA Waraibu wa dawa za kulevya, kimsingi ni watumiaji vilevi hivyo na wanaofahamu mengi yanayowasibu na namna wanavyopambana kuishi kawaida.

Wakizungumza na Nipashe, kwa kina, wakiwa wamegawanyika katika makundi matatu, ikiwamo linaloitwa Vipumbaza. Hao wanahusishwa na dawa aina 'heroine' na 'methadone' zinazomfanya mtu asinzie muda mrefu mara nyingi, mwili ukikosa ufanisi wa kushughulika.

Pili,Vileta Njozi; vinajumuisha watumiaji bangi na uyoga. Vyote humfanya mtumiaji kuchukulia vitu tofauti na uhalisia wake, vinaondoa aibu na kuwafanya wathubutu kufanya lolote kwa kujiamini.

Tatu ni Vichangamshi, kundi la watumiaji dawa aina cocaine na vinywaji vyenye nicotine, vyote ni vya kujifurahisha.

**ASIMULIA YANAYOMSIBU**

Dismas Mwendapole, mkazi wa Yombo- Kilakala, Dar es Salaam, amefanikiwa kuacha dawa za kulevya na sasa yuko katika tiba mbadala ya dawa 'methadone' baada ya kuacha dawa hizo, anashauri wapatiwe kazi za kufanya kiuchumi, ziwasadie.

"Mwaka 2008 baada ya kumaliza kidato cha nne nilipata daraja la nne kwa alama 28. Nilikosa ndugu wa kunilipia ada, sikuendelea na masomo, ndoto yangu ya kuwa mwandishi wa habari na mtaalamu wa kompyuta ilizimika.

"Nilikwenda Zanzibar kutafuta maisha, nikawa mzururaji wa ufukweni (beach boy) kusubiri wazungu (watalii) kuwalaghai na kuwatembeza mjini kisha nilikuwa najipatia pesa kidogo dola za Marekani 20 sawa na shilingi 20,000 kununua chakula na matumizi mengine," anaeleza.

**ALIVYOANZA MAISHA YA 'UNGA'**

"Nilipokuwa Zanzibar maisha yaliendelea, mmoja wa marafiki zangu niliokuwa nashinda nao ufukweni alikuwa anatumia dawa za kulevya akanishawishi nitumie kuondoa aibu, niweze kuwachangamkia Wazungu nikaingia mtegoni, haikuwa tabu sana kuanza kwa kuwa nilipokuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari nilikuwa navuta bangi.



Mkurugenzi wa CPHEO Banza Omary Banza akiwa ofisini kwake.

"Nilianza matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya kuchanganya unga wa heroine na tumbaku (cocktail) kwenye karatasi maalumu ya Lizza na kuvuta kama sigara. Sikuwahi kujidunga sindano wala kuvuta unga kwa njia ya pua," anasimulia.

**MAISHA MAPYA YALIVYO**

Mwendapole anaeleza ametumia dawa za kulevya pasipo kujua madhara yake wala kuzingatia matumizi salama hadi mwaka 2010 aliporejea jijini Dar es Salaam, akakutana na wafanyakazi wa shirika la Medicins du Monde (MDM).

Anataja moja ya jukumu lake ni kuhamasisha matumizi salama ya dawa za kulevya, kwa kuwapatia watumiaji mabomba ya sindano, pia kuwahudumia wanapopata maradhi akiwapa mafunzo ya sanaa na ufundi, kuwadhamini polisi, inapotokea wamekamatwa kwa uhalifu.

"Mafunzo ya sanaa yalisaidia kunitoa kwenye kufanya uhalifu wa uporaji na wizi, japo nilitumia kipaji changu cha sanaa ya kuimba na kutunga nyimbo kuwatapeli watu, kwa kuwaomba wanipe pesa za kwenda kurekodi studio, zikawa zinaishia kununua kete za heroine.

"Nilibahatika hadi kufika kwa wasanii wa TMK Wanaume lakini niliishia kuwaibia flashi, CD na vifaa vingine vya studio nikafukuzwa," anasema.

Mwendapole, mtunzi na mwandishi bora wa hadithi na riwaya, anakiri ni muumini mzuri, pia mwenye, historia kuangukia tabia udokozi, ulaghai na utapeli, ili kupata pesa za kununua dawa za kulevya na hawezi kuvumilia magumu ya kuzikosa walau kwa muda mfupi.

"Waraibu hukosa uaminifu, wanapokosa pesa huweza kufanya lolote hata kumdhuru mtu ili wapate pesa za kununua dawa za kulevya," anasimulia.

**ALIVYOFANIKIWA KUACHA**

Mwaka 2016 Mwendapole anasimulia akakutana na aliyekuwa mfanyakazi wa shirika la MDM Kitwara Nginila, hata akamuingiza kwenye mradi wa kutengeneza video za miradi (Participatory Video Projects-PVP) na masuala ya kompyuta.

Anasimulia baada ya kuonyesha mwitikio, Nginila akaamuunganisha na mwanasaikolojia Benjamin Myovela, aliyesaidia kumbadili, kuanzia kumshauri namna ya kuacha, akianza na kupunguza muda na kiwango cha utumiaji heroine.

"Mwaka 2017 nilipata mfadhili mwanamke kutoka Holland, akanipeleka 'South Beach Sober House' na kunilipia. Nikaanza maisha mapya ya kutotumia chochote, hakuna sigara, bangi wala pombe ukiwa kule. Kuanzia asubuhi, ni kupewa elimu tu!

"Nilipambana na 'arosto' (kuishiwa pesa) maumivu yalikuwa makali nilitamani kukimbia toka 'sober house' kama nilivyoshuhudia wengine wakifanya, lakini nilivumilia na kuamua kukaa kule hasa nikimfikiria aliyenilipia pesa zake shilingi 900,000 kwa miezi mitatu (kila mwezi Sh. 300,000.

"Kwa sasa mimi ni muelimishaji rika toka Community Peers for Health and Environment Organization (CPHEO) tunafanya kazi ya kutoa elimu na huduma za upunguzaji madhara kwa watumiaji dawa za kulevya kwenye masikani wanamoshinda.

"Changamoto kubwa tunapata toka kwa wauzaji wa unga wamekuwa wakituchukia na kutuandama sisi tunaohamasisha vijana kuacha dawa, wanadai tunawaharibia biashara na kuwafukuzia wateja wao," anabainisha Mwendapole.

Kwa msaada wa shirika la MDM lililodumu hadi mwaka 2018, Mwendapole anasema amewezeshwa kuhudhuria mkutano wa siku 21 uliofanyika jijini Vilmis nchini Lithuania mwaka 2013, ikihusisha makundi maalumu; watumiaji dawa za kulevya; kinadada wanaojiuza; na wenye VVU.

Hapo inalenga kujadili namna ya kutokomeza maambukizi ya VVU kufikia asilimia 90, kujitahidi kufubaza makali yake na kuwa na asilimia 90 ya wanaojua hali zao za maambukizi ya ukimwi, kufikia mwaka 2020.

**MKURUGENZI WA CPHEO**

Banza Omary Banza, ni Mkurugenzi wa CPHEO, cheo alichopata baada ya kuamua kuacha kutumia dawa za kulevya aina ya heroine na

kuwa miongoni wa waraibu wanaotumia tiba methadone kwa takriban miaka mitano sasa, tangu 2017 ikiwa ni mbadala wa dawa za kulevya.

Ameanzaje matumizi ya dawa za kulevya? Hapo anajibu ni alipomaliza shule na kutafutiwa kazi katika uwanja wa ndege na mwaka 1997 akaanza kutumia dawa hizo, baada ya kupata rafiki anayeziuza akimkaribisha chumbani kuliko andaliwa na kufungwa dawa hizo.

"Nilianza kuonja na hatimaye kuwa mraibu. Nilikuwa ninatumia kwa njia tunayoiita 'cocktail'. Hii hufanyika kwa kuchanganya unga wa heroine kwenye sigara, kisha inawashwa kwa moto na kuvutwa, moshi na unga huingia ndani na kutokea puani," anasimulia.

Banza anaendelea: "Sikuweza kuzingatia kazi kwa kuwa muda mwingi nilikuwa najishughulisha na matumizi ya dawa za kulevya. Hali hiyo ilifanya niachishwe kazi, pia nilifukuzwa pale nilikokuwa naishi.

"Nilitumia dawa ya kulevya kwa zaidi ya miaka 20, katika kipindi hicho nilikutana na vitu vingi sana pamoja kushindwa kuihudumia familia yangu (mke na mtoto). Mbaya zaidi, nilikaa mahabusu zaidi ya mara tatu kwa nyakati tofauti, kutokana na kushiriki katika uhalifu...ikiwamo wizi."

**BAADA YA KUBADILIKA**

Banza anasimuilia baada ya kutumia mbadala methadone, kumemsaidia kimaisha, anahudhuria hospitali kwa tiba ya muda mrefu, kati ya miaka miwili hadi nane.

"Wapo waraibu wanaoshindwa kuacha kwa kushindwa kujiamini kuwa wanaweza kuishi bila 'stim' ya dawa za kulevya hao hutumia kwa muda mrefu hadi miaka nane," anaeleza.

Banza anaeleza: "Mwaka 2010 nilijiunga na Kituo cha Video kwa Afya na Maendeleo (VAMA) kilichoanzishwa na taasisi ya MDM kwa lengo la kutoa huduma za afya, chakula, mafunzo sanaa na ujasiriamali kwa waraibu wa dawa za kulevya."

Pia, anasema mwaka 2017 kituo hicho kilibadilishwa jina na kuwa CPHEO, yeye akatwaa ukurugenzi, akidokeza asilimia 90 ya viongozi na wanachama wetu ni waraibu wa dawa za kulevya.

"Tulianza kujitolea kwa kufanya 'mobilization' kwa waraibu tukishirikiana na wataalamu wa afya, tunapita maskani za waraibu ku-

ENDELEA UK. 13

AFYA

# LHRC, JICA waingia ubia vita ukatili kijinsia na ngono zembe

## • Wanafunzi katika utetezi wa kipekee

**Na Sabato Kasika**

HADI sasa Dar es Salaam kumeanzishwa harakati kukabili udhalilishaji, unyanyasaji na ukatili kingono vinavyotajwa kukithiri ndani ya jamii.

Wajumbe wa Kamati ya Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ya mkoa huo, wamekutana na kuazimia kufuatilia vitendo hivyo, kuanzia ngazi ya familia.

Mwenyekiti wa Kamati, Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Rashid Mfaume, ametangaza wiki iliyopita katika mkutano kutambulisha mradi wa majaribio kukomesha madhila hayo katika Kata za Makumbusho na Mwananyamala, wilayani Kinondoni.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga, anawaambia wajumbe wa kamati hiyo akielezea hali halisi ilivyo wilayani humo, ambayo baadhi ya wajumbe wake ni polisi, wanasheria, mahakimu, viongozi wa dini na madaktari.

Pia, kuna wengine kutoka ngazi ya chini kwenye jamii, wenye jukumu la kuhakikisha vitendo hivyo vinakoma. Anaendelea: "Ni wazi vitendo hivi vitakuwa vingi mkoani kwetu, hasa kwa kuzingatia Dar es Salaam ina watu wengi."



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, akizungumza katika Mradi wa Majaribio Kukomesha Ukatili Jinsia katika Jamii wilayani Kinondoni, wiki iliyopita. **PICHA: SABATO KASIKA.**

### HALI INAYOTAWALA

Henga ambaye pia ni wakili, anasema ukatili wilayani Kinondoni umekithiri kukiwapo jumla ya kesi 57,626 na kati yake, mengi ni udhalilishaji na ukatili kijinsia, hasa ngono.

"Yapo makundi maalumu yanayojumuisha watoto, watu wenye ulemavu na wanawake yameathiriwa zaidi na janga la ugonjwa wa corona mwaka 2020, ambalo lililazimu serikali kufunga kwa miezi mitatu," anasema Henga.

Anaeleza utafiti wa LHRC umebaini kipindi hicho kuliripotiwa kongezeka matukio ya ukatili; kuanzia mwaka 2018 hadi 2020 kituo hicho kilikusanya zaidi ya matukio 2,991 ya mimba za utotoni yaliyoripotiwa katika mikoa mbalimbali.

"Mwaka 2020, LHRC ilikusanya (ripoti) matukio 448 ya mimba za utotoni, ambayo yaliripotiwa katika mikoa 15 ya Tanzania Bara kuanzia Januari hadi Desemba, matukio mengi yalihusisha wasichana wenye umri wa miaka 13 hadi 17.

"Wasichana waliopata mimba walilazimika kuacha shule na kupoteza haki yao ya elimu na kufanyiwa vitendo vya kibaguzi," anasema.

Anafafanua LHRC iliamua kuingia makubaliano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kufanya mradi wa majaribio kuwajengea uwezo na kuhamasisha wadau kuzuia na kukabiliana na udhalilishaji kingono kwa makundi mbalimbali, kisha kufanya tathmini jinsi ya kuandaa programu zenye tija na ufanisi kukomesha vitendo hivyo.

"Mradi huu unatekelezwa katika Hospitali ya Mwananyamala ambayo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dar es Salaam na jamii inayoizunguka zikiwamo kata za Mwananyamala na Makumbusho," anasema.

### MAVUNO YAKOJE?

Henga anasema wameshafundisha watumishi zaidi ya 200 wa Hospitali ya Rufani Mwananyamala, pia polisi zaidi ya 50 wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Mkoa wa Kipolisi Kinondoni.

"Wengine waliopata mafunzo ni watendaji na wenyeviti wa serikali za kata na mitaa katika mitaa yote 13 ya kata za Mwananyama na Makumbusho,"anasema.

Anaendeleza orodha kwamba ni: "Wajumbe zaidi ya 50 wa MTAKUWWA ngazi ya mtaa na kata, maofisa watendaji wa serikali ngazi ya mkoa, kata na mtaa na wanaharakati ngazi ya jamii wakiwamo wa asasi za kiraia."

Pia, anaeleza mradi umetembelea vituo 11 vya kipolisi kati ya 13 vilivyopo, ili kujenga uwezo zaidi kwa watendaji wa Dawati la Jinsia na Watoto na umewezesha Hospitali ya Mwananyamala kutenga chumba maalumu cha kuhudumia manusura wa ukatili kingono.

"Mradi pia umewezesha Hospitali ya Mkoa kuandaa utaratibu maalumu wa kufanya uchunguzi kwa manusura wa ukatili, awali kulikuwa na mtaalamu mmoja wa maabara kuchunguza, huku kesi nyingi ushahidi ukipotea na sasa wataalamu ni watatu wanaotakiwa kuthibitisha vipimo.

"Tunafikiria kuweka mwanasheria katika Kituo cha Mkono kwa Mkono (cha ziada) huku kikiendelea kuchagiza serikali na wadau kuweka mwanasheria wa kudumu kama ulivyo mwongozo wa uanzishaji wa vituo hivyo," anasema Henga.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Zavery Benela, anaunga mkono hoja kwamba, wataendelea kushirikiana kwa karibu na LHRC, ikizingatiwa watumishi wengi hawakuwa na uelewa wa mengi katika eneo hilo, akiahidi kuendelea kushirikiana na LHRC.

### MWANASHERIA ALAUMU

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Adolf Kissima, anasema vita ya kukomesha vitendo hivyo inahitaji ushirikiano wa karibu kuanzia manusura hadi ndugu zao.

Analalamika baadhi ya kesi zinakwama kwa kukosa ushahidi, wahusika wakimalizana nje kabla ya mahakama, hata kesi inaishia kufutwa.

Mrakibu Mwandamizi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalumu ya Dar es Salaam Leah Mbunda anaeleza: "Wapo wazazi na walezi ambao watoto wao wakifanyiwa vitendo hivyo na ndugu zao huwahamishia vijijini kuficha aibu au kuwaonea huruma watuhumiwa."



Dismas Mwendapole, aliyefanikiwa kuacha dawa za kulevya, akitoa elimu kwa kundi rika juu ya namna bora ya kuacha kuzitumia. **PICHA ZOTE: DEVOTA MWACHANG'A**

# Simulizi tata za watumiaji dawa kulevya, safari ngumu kuziacha

**INATOKA UK.12**

wahamasisha kupima TB tunachukua 'sample' (sampuri).

"Tunatoa elimu kuhusu kuacha matumizi ya dawa za kulevya, kuwashawishi waanze kutumia methadone, pia kuwashuri juu ya utatuzi masuala ya kisheria," anaeleza Banza.

Kuhusu kuendeleza asasi, ameshawasilisha maombi sehemu mbalimbali zikiwamo ubalozi wa Marekani na shirika la Uhai Kenya linaloshughukia makundi maalumu kama waraibu dawa za kulevya.

### MTAALAMU WA AFYA

Latipha Masasi, mtaalamu wa afya kutoka Kata ya Tandika wilayani Temeke, anasema jamii inapaswa kujihusisha katika utoaji misaada kwa makundi maalumu, wakiwamo watoto yatima, wajane, wenye VVU, pia waraibu wa dawa za kulevya.

Anawataja waraibu ni sehemu ya jamii ambao , wakisimamiwa kwa ukaribu, wanabadilika kuwa raia wema wanaopendwa na umma.

Latipha anasema huwa anawaandalia chakula na kuongea na kujua matatizo yao, kuwashawishi na kuwapatia huduma za vipimo vya afya hasa wajawazito.

"Mimi mtaji wangu ni watu sio pesa. Ninahudumia makundi maalumu kuwapatia msaada wa huduma ya afya ya uzazi, kupima VVU na TB; pia ninashirikiana na kinamama 9,208 (mama lishe na walemavu)....," anasema.

Diwani Kata ya Tandika, Uzairu Athuman, ana maoni yake: "Nimefarijika sana kuona Mama Latipha kaguswa na makundi haya na kuhamasika kusaidia kwa kuwaunganisha wakinamama na kuhamasisha jamii iwasaidie bila kuwabagua."

MAZINGIRA

## MADHILA YA MIGODINI....

# Vifo vya wachimbaji kufunikwa na vifusi vinavyotawala Katavi

- Kisa? Kuna wanaoingia kinyemela usiku
- Migodi imechoka, miaka 40 inatumika
- Wachimbaji, Ofisa Madini, Polisi wanena

**Na Neema Hussein, KATAVI**

HADI sasa vifo vitokanavyo na kufukiwa na vifusi kwa wachimbaji wadogo, chanzo chake kimekuwa kitendawili, licha ya elimu kutolewa kwa wataalamu wa madini, hasa katika namna ya kujikinga na janga hilo.

Ni hatua inayofikiwa ya lengo la serikali na wataalamu wa madini kupunguza au kuondokana kabisa na vifo hivyo vya wachimbaji wadogo.

Nipashe ilitaka kufahamu chanzo cha wachimbaji wadogo kufukiwa na vifusi wakiwa ndani ya shimo la dhahabu, ikiwa ndio kazi waliyochagua kwa lengo la kujipatia kipato.

Kwenye machimbo ya Dilifu yaliyoko katika Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, mchimbaji mdogo Salumu Hamisi anayetoka kikundi cha Kagera Group, kwenye machimbo hayo, anasema hali duni ya maisha inawasababisha kufanya kazi hata sehemu zilizozuiliwa na hata kuhatarisha maisha yao, akiwa na ufafanuzi kwamba eneo wanalochimba dhahabu limechoka kutokana na kuchimbwa muda mrefu.

Anaendelea kufafanua: "Viongozi wa kikundi chetu cha Kagera Group huwa wanatuhimiza sana tuangalie sehemu tunazofanyia kazi. Tusipige zile nguzo zinazokuwa ni mhimili wa duara, kuufanya mduara kuanguka na kutufunika tulio ndani.

"Kuna vifo aina mbili hapo kuna wanaofunikwa na vifusi na kuna wanaokufa kwa kukosa hewa, yaani wameingia duarani, duara ambalo limekaa muda mrefu bila kufanyiwa kazi, sasa limeishaingiza ile hewa chafu, unapoingia tu unakosa hewa safi na unapoteza maisha.,"





Ndivyo ilivyo shughuli za machimbo zikiendelea mkoani Katavi. **PICHA ZOTE: MTANDAO,**

### WACHIMBAJI WADOGO

Nobert Protasi, ni mchimbaji mdogo katika machimbo hayo anayesema serikali iwasaidie kungana na kikundi hicho kuondoa ardhi iliyochoka, ambayo imechimbwa kwa muda mrefu hadi kuifikia ardhi mpya itakayokuwa salama kwao kufanya kazi hiyo.

"Kuna wakati watu huwa tunapata hofu sana na tunakuwa ni watu wenye majonzi, ila tu ndio hivyo kutokana na hali zetu tunaendelea tu kuchimba. Ndiyo maana mimi nasema serikali itupigie 'trencha' hapo, yaani ituletee 'skaveta' itukwangulie huo mlima, hayo maduara yote yatupwe ili tuanze kuchimba ardhi mpya ambayo ni imara," anafafanua Protasi.

Gabriel Boniface, Mweka Hazina wa Kikundi, ambaye pia ni mchimbaji, anaiambia Nipashe kwamba eneo hilo limechimbwa zaidi ya miaka 40 sasa, hivyo limechoka na kusababisha vifo vya kila mara.

"Sababu nyingine ni wachimbaji wenyewe kukaidi, wanapoambiwa wasifanye kazi kwenye duara fulani ambalo limezuiliwa na kuzungushiwa kamba, lakini wanafanya usiku kwa wizi.

"Hawa wa hivyo wanaitwa 'manyani.' Unakuta wanaingia kwenye shimo usiku kufanya kazi, matokeo yake shimo linaanguka wanafukiwa na kufa," anafafanua mchimbaji huyo.

Emmanuel Ernest, mjumbe wa kikundi hicho anasema eneo analotaja la Dilifu, lina dhahabu za kutosha na kinachowashinda kuzifikia ni kukosekana vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi, hali inayochangia vifo vya watu.

Katika hilo, ombi lake ni serikali iwape msaada wa vifaa vya kisasa ili waondokane na uchimbaji wa kizamani na hata waweze kuzalisha madini mengi zaidi.

Anafafanua: "Hivyo, vifo vinatokea sana kipindi hiki cha mvua, mfano duara limekaa pembe nne, sasa ili wachimbe kuna miti huwa inapangwa pembeni ya duara kwa usalama zaidi. Unakuta ardhi ya kushika hiyo miti imelowa maji na kutitia, kama kuna watu wako chini wanapata ajali kwa njia hiyo."

### MNUNUZI WA DHAHABU

Justine Francinsco, ni mnunuzi wa dhahabu katika machimbo hayo, anayekubaliana na hoja kwamba ameshawahi kushuhudia vifo hivyo na vinawaathiri kiutendaji, ikiwamo kupunguza nguvu kazi katika eneo hilo.

"Kwakweli hali ilikuwa ni ya kutisha, kila mtu alikuwa anaogopa maana kuna wengine walikuwa wameumia vibaya, wamevunjika viungo mbalimbali vya miili yao, lakini kuna wengine wanakuwa wanakufa kwa kukosa hewa safi, wao wanakuwa hawana majeraha," anaeleza shuhuda huyo.

### OFISA MADINI

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Katavi, Andrew Mwalugaja, anafafanua kwamba chanzo kikubwa cha kiufundi kwa wachimbaji kufukiwa ni udhaifu wa miamba hasa katika kipindi hiki cha mvua.

Mhandisi Mwalugaja, anaeleza kila mara huwa wanakagua na kutoa elimu kwa wachimbaji pamoja na kuwashauri kuweka magogo ya kusaidia kudhibiti duara au shimo lisianguke.

Mwalugaja amesema takwimu zinaonyesha ndani ya miaka miwili kati ya mwaka 2020 na 2021, watu 10 wameshapoteza maisha kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kufukiwa na vifusi, kukosa hewa safi ndani ya shimo na kuteleza kutokana na magogo yanayozuia shimo kulowa maji

Anataja mnamo Agosti mwaka 2020 katika machimbo ya Dilifu, mtu mmoja alipoteza maisha na mwezi uliofuata Septemba katika machimbo ya Ntumba, nako mtu mmoja alifariki.

Pia, anaeleza kuwa Mei mwaka jana katika Machimbo ya Mtisi, watu watatu walipoteza maisha, Agosti mwaka jana watu wawili walifariki na mwezi uliopita mtu mmoja.

### RPC ANENA SHIDA ZA VIFO

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Hamad, ameiambia Nipashe kuwa katika kipindi cha miaka mitatu, vimetokea vifo 24 vya wachimbaji wadogo vikisababishwa na kufukiwa kwa vifusi.

Anafafanua kuwa chanzo cha vifo hivyo, ni miundombinu duni iliyoko hasa katika kipindi cha mvua ardhi inakuwa imelowa, hivyo kuwafunika wachimbaji walioko ndani ya mashimo hayo ya madini ya dhahabu.

Kamanda Hamad anasema, mikakati yao polisi ni kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo namna ya kujikinga na vifo hivyo na kuweka doria ya kuwadhibiti wachimbaji wanaofanya kazi kwa wizi usiku, ambao ni maarufu kwa jina la 'manyani.'





## Chama chatakiwa kutetea maslahi ya wanajeshi wastaafu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa Chama cha Muungano wa Wanajeshi Tanzania (MUWATA), wametakiwa kutetea maslahi ya wastaafu badala ya kujivunia nafasi walizochaguliwa na kusababisha migogoro isiyo na tija.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Kanali Mstaafu Mahamud Mshamu Lwimbo, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wanachama baada ya kufanyika uchaguzi wa chama hicho jijini hapa.

Alisema ni vyema viongozi wanaochaguliwa kutokuwa kikwazo cha maendeleo ya chama hicho na kuwa mstari wa mbele kutatua kero za wanachama wao. Kanali Lwimbo alisema chama hicho tangu kuanzishwe miaka 11 iliyopita hakina mafanikio kutokana na waliokuwa wanakiongoza madarakani, kutotimiza majukumu wajibu wao.

"Kwa kipindi cha miaka 11 chama kimekuwa hakina maendeleo zaidi ya kuvutana na kusababisha migogoro isiyokuwa na tija na maendeleo, sasa niombe uongozi huu tuliochaguliwa tuelekeze fikra zetu kutatua kero za wastaafu badala ya kujivunia nafasi hizi na vyeo suala ambalo limepitwa na wakati kwa wakati huu," alisema Lwimbo.

Alihimiza kuwa wabunifu wa kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo na wanachama wake wajishughulishe na ujasirimali ili kujikwamua kiuchumi.

"Chama chetu kina karibu wataalamu wengi wa aina mbalimbali na hakuna sababu ya kutoibua miradi ambayo inayoweza kutuingizia kipato, ukizingatia kuwa kila fani tunaifahamu na tunaiweza kuifanya, hivyo kwa uongozi huu tusikubali kuongoza chama kwa umaskini wakati fursa ya miradi mingi ipo," alisema.

Kwa upande wao, wanachama wa MUWATA waliutaka uongozi uliochaguliwa kuongoza kwa hekima na busara, ili kuepukana na migogoro isiyo kuwa tija itakayokigawa chama.

Meja Mstaafu Hussen Mzee Chiche, alisema wanatarajia kuona wanavushwa kwenye hali ya umaskini hadi kufikia hatua ya kiuchumi, na siyo kuongeza migogoro, ambayo imekuwa ikikwamisha maendeleo ya chama.

Waliochaguliwa ni Mwenyekiti Taifa Kanali Mstaafu Lwimbo, Makamu Mwenyekiti Taifa Luteni Kanali Mstaafu Justus Issack Anthony, Katibu Mkuu Taifa Sajini Mstaafu Taji Dauka Njelekela, Katibu Mkuu Msaidizi Taifa Sajini Mstaafu Nassoro Masoud Nassor na Mtunza hazina Taifa,
Koplo Mstaafu Arafa Mwinyi Nemshi.

# Masjala hewa ya ukaa kuanzishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imejipanga kuanzisha masjala hewa ya ukaa itokanayo na misitu huku ikihimiza wananchi kutambua umuhimu wa kupanda miti.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk.Damas Ndumbaro, aliyasema hayo juzi jijini hapo alipokuwa akiongoza zoezi la upandaji miti eneo la Iyumbu ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Uzinduzi wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2021.

Alisema masjala hiyo itaweka misitu yote inayotaka kufanya biashara ya hewa ukaa ambapo zitapatikana fedha nyingi na kuchangia uchumi wa nchi.

"Kuna watu sasa wameanza kuvuna hewa ya ukaa na wanapata fedha nyingi sana kijiji kinapata mabilioni kwa sababu ya hewa ya ukaa hii ndio faida ya misitu, " alisema.

Alisema wizara hiyo kupitia Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) wamejipanga kuifanya Tanzania yote kuwa ya kijani kwa kulinda misitu iliyoko isiharibiwe au kukatwa ovyo.

"Tukikata miti lazima tupande miti ili kuifanya Tanzania kuwa ya kijani, kuna faida nyingi za misitu, kuna watu wanaishi kwa ajili ya kupanda misitu na hata nchi zingine misitu inachangia kiwango kikubwa sana kwenye GDP," alisema.

Alibainisha kuwa kwa Tanzania asilimia 3.5 ya GDP inazidi sekta nyingine kutokana na umuhimu wa misitu.

Alisema asilimia 54 ya eneo la Tanzania ni misitu zaidi ya hekta 400,000 ni misitu na inatunzwa kupitia TFS na wananchi kwa ujumla.

"Suala la misitu kwetu sisi ni vita, suala la misitu kwetu sisi ni kipaumbele, hatuzuii mkaa ila tunataka kujua umekata wapi kwa kibali kipi? Lakini kama huna nyaraka hizo wewe ni mharibifu, tunafanya hivyo kwa faida ya Watanzania wote," alisema.

Aidha, alisema milima iliyoko Dodoma yote itakabidhiwa kwa TFS kwa ajili ya kupanda miti na kuitunza ili kujiepusha na kuvamiwa na kujengwa ovyo.

"Sisi Wizara na TFS tutahakikisha Dodoma linakuwa jiji la ukweli maana ni Makao Makuu, tutatizimiza wajibu wetu kufikia azma hii," alisema.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mary Maganga, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kupanda miti kwenye makazi.

Naye Mkurugenzi wa Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba, alisema miongoni mwa mambo yaliyoko kwenye sera hiyo mpya ni masuala ya utunzaji wa rasilimali za misitu.

Alisema kutokana na jitihada zinazofanywa na serikali pamoja na wadau mbalimbali ambapo imeendelea kuhifadhi maeneo ya misitu na asilimia 62 ya maeneo nchini yamehifadhiwa.

Kwa upande wake, Kamishna wa Hifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema wiki hiyo inatumika kupanda miti kwenye maeneo yaliyopoteza uoto wa asili.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
(AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 08 OF 2022

THE REPUBLIC
VERSUS

WEN XING PLASTIC CEMENT INVESTMENT CO. LIMITED........................................ACCUSED PERSON

To:
Yang Jiwen & Xia Lin
Directors / Shareholders
Wen Xing Plastic Cement Investment Co. Limited
Plot No. 55, Kibaha Industrial Area
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of March 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 3rd day of February 2022

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name.......................................

Signature.......................................

Qualification/Relationship
Date.......................................

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 182 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

MADOSHI ELISHA KADASHI........................................ACCUSED PERSON

To:
Madoshi Elisha Kadashi,
Kibululu Street, Goba Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 17 day of FEBRUARY 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25 day of JAN. 2022

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name.......................................

Signature.......................................

Qualification/Relationship

Date.......................................



## HABARI MBEYA

# Tanzania yaibuka kidedea mapambano dawa za kulevya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imeibuka kidedea kwa kupambana na dawa hizo baada ya kutangazwa na Umoja wa Mataifa kufikia asilimia 90 ya mapambano.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alisema juzi katika kikao chake na wadau ya kupambana na dawa kilichofanyika juzi jijini Mbeya alisema hatua ya Tanzania kupata sifa hiyo ni kutokana na jitihada inazofanya.

Alisema mamlaka mbalimbali za Umoja wa Mataifa zilizokuwa na jukumu la kuchunguza namna Tanzania inavyopambana na dawa za kulevya, ziliamua kuipatia Tanzania asilimia 90.

Kusaya alisema mbali na kupewa asilimia 90, aliwapongeza Watanzania kwa kuendelea kupeana elimu juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya.

"Tunawashukuru Watanzania kwa kuungana pamoja katika vita hii dhidi ya dawa za kulevya. Tumeshuhudia ndugu, jamaa na marafiki walioathiriwa na dawa hizo na kupoteza nguvu kazi ya taifa. Nawaahidi mamlaka hii itaendelea na jitihada kuongeza kasi ya kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na hatimaye kufikia asilimia 100," alisema Kusaya.

Pia alisema katika kipindi cha mwaka 2021 kuanzia Januari hadi Desemba, mamlaka ilikamata kilogramu 930 za dawa mbalimbali za kulevya.

Kusaya aliongeza kuwa wanaendelea kufanya misako maeneo mbalimbali nchini na kwamba hawataogopa kiongozi yeyote ambaye atabainika kutumia au kusafirisha dawa za kulevya na kwamba atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema katika dawa za kulevya, bangi ndiyo inaongoza kwa kutumiwa na vijana wengi nchini.

Dk. Chuachua alisema madhara yake ni kuongezeka kwa kizazi cha vijana ambao hawana tija kwa jamii na taifa kwa ujumla. Aliwataka vijana kuachana na makundi yasiyofaa badala yake wajikite kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza ndoto zao.

Mratibu wa Shirika la Walter Reed, Wahija Mzee, alisema miongoni mwa vitu vinavyochangia kasi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI ni matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema dawa za kulevya ni miongoni mwa visababishi vikubwa ya maambukizi ya Ukimwi kwa kuwa wanaotumia hushindwa kujitambua na kujiepusha na vishawishi.

Mzee aliongeza kuwa miongoni mwa mikakati ya kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevya ni kuongeza vituo vya kuwasaidia waathirika hao katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ili kupata matibabu na kupona kabisa.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wapili kushoto) na ujumbe wake, walipomtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma jana. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Filbert Mponzi na Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali, Alfred Shao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja 2,500 waunganishiwa umeme vijijini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATEJA 2,508 wa wilaya tano za Mkoa wa Mbeya, wameunganishwa na nishati ya umeme kupitia mradi wa umeme vijijini awamu ya tatu unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA III) mzunguko wa pili.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Mbeya, Mathias Songolo alisema juzi kuwa Sh. bilioni 40 zilitumika kukamilisha mradi huo.

Alibainisha kuwa katika Wilaya ya Mbeya vijiji 32 viliunganishwa na umeme na kuwafikia wateja 704, Chunya vijiji 12 wateja 264, Kyela vijiji 26 wateja 572, Mbarali vijiji 17 wateja 374 na Rungwe vijiji 27 wateja 704.

Mhandisi Solongo alisema mradi huo ulitekelezwa na mkandarasi M/s ETDCO Transmission and Construction and Maintainance Company kampuni ambayo inamilikiwa na serikali huku msimamizi akiwa TANESCO na mhandisi mshauri Aries International.

Aidha, Songolo alivitaja vijiji vya mkoa wa Mbeya vilivyosahaulika kwenye REA III mzunguko wa II kuwa ni 39 vyenye jumla ya wateja 770.

"Mbali na kuwasaidia wananchi kupata nishati ya umeme, TANESCO tumesaidia kuinua kipato kwa wananchi wa vijiji kwa kuanzisha biashara ndogo ndogo kama vile saluni, uuzaji vinywaji baridi na sehemu za kuonyeshea mpira," alisema Songolo.

Alisema TANESCO inajivunia kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kama vile visima vya maji, mashine za kukoboa na kusaga nafaka

Matarajio ya shirika hilo, alisema ni kwamba baada ya kukamilika kuunganisha huduma ya umeme katika vijiji vyote vya mkoa wa Mbeya, kutakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi ikiwamo kuchochea na kuibua fursa za kiuchumi kama vile uanzishwaji wa viwanda vidogo vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao.

## Mil. 631/- kutatua tatizo sugu la maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI imetenga Sh. milioni 631 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji ambao utajengwa katika Kata ya Itamboleo utakaohudumia zaidi ya wakazi 20,000 wa eneo hilo na maeneo jirani.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliowahusisha wananchi wa Itamboleo na mkandarasi ambaye aliingia mkataba wa utekelezaji wa mradi huo.

Alisema fedha hizo zilizotolewa na serikali kutokana na mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya mapambano ya UVIKO- 19, zinalenga kutatua tatizo la maji kwenye kata ya Itamboleo.

"Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ametuletea Sh. milioni 631 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji unaojengwa katika Kata ya Itamboleo, zitapatikana fursa mbalimbali ikawamo ajira kwa wanakijiji," alisema Mfune.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Samuel Hechei, alisema juzi kuwa mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili na kwamba awamu ya kwanza utahusisha ujenzi wa banio, tangi la lita 300,000, vituo vinane vya kuchotea maji na ujenzi wa mtandao wa mabomba kilomita 15.9.

Alisema awamu ya pili, mradi utatekelezwa katika vijiji vya Matebete, Mbalino na Kapunga na itahusisha ujenzi wa mtandao wa mabomba kilomita 72.2, tangi la lita 200, 000 na ujenzi wa vituo 19 vya kuchotea maji na kwamba utagharimu Sh. milioni 3.9.

Akizungumzia mradi huo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbarali, Hashimu Mwalyawa, alimpongeza Mkuu wa Wilaya kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Pia alimpongeza kwa kuleta mradi wa maji Kata ya Itamboleo kwa kuwa walikuwa na shida ya maji hatimaye pesa zimetengwa kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano katika kutekeleza ujenzi wa mradi huo na kuwasihi kuepukana na vitendo vya wizi wa vifaa hivyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, ambaye ni Diwani wa Kata ya Itamboleo, Twalib Lubandamo, alisema eneo hilo lilikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji na kwamba mradi huo utasaidia kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema mkataba wa utekelezaji wa mradi ulitiwa saini Januari 10, mwaka huu, na unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi sita na kwamba ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi 22,543.





# Wawakilishi UN, makatibu wakuu wizara wakutana kujadili mafanikio, changamoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAWAKILISHI wa mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN), wamekutana na makatibu wakuu wa wizara katika serikali ya Zanzibar, kujadili mafanikio yaliyopatikana kupitia usaidizi wa umoja huo na mipango ya utekelezaji.

Akizungumza katika mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa Baraza la Mapinduzi, Forozani mjini Zanzibar, Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Zlatan Milisic, alisema mkutano huo utajadili Mfumo wa Ushirika wa Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa (UNSDCF) ambao unaeleza nia yake katika kuendeleza vipaumbele vya maendeleo kwa Zanzibar.

Alisema UN itaendelea kusaidia Zanzibar kufikia ajenda ya 2030 kwa maendeleo endelevu na ajenda ya Afrika 2063.

Alisema UN iliunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutimiza dira yake ya taifa ya mwaka 2020 ambayo miongoni mwa mafanikio yake ni Zanzibar kuwa nchi ya kipato cha kati.

"Kwa kujua UN inafanya nini Zanzibar, tunaweza kuwasiliana kwa sauti moja juu ya mafanikio na kuwa na uwazi wa changamoto zinazofanana. Hili ni jambo la msingi katika moyo wa ushirikiano na ni muhimu katika kupanua ubia na msingi wa rasilimali za washirika wa maendeleo Zanzibar," alisema.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mussa Haji, aliipongeza UN kwa kuwa mshirika wa maendeleo na kuunga mkono mipango ambayo italeta mabadiliko Zanzibar.

"Hizi ni pamoja na msaada wa kuondoa umaskini uliokithiri, kupunguza kukosekana kwa usawa, kulinda mazingira, kukuza uwezeshaji wa wanawake na kuwezesha maendeleo endelevu kwa Wazanzibari wote," alisema.

Pia alisema mkutano huo ni utaratibu mzuri wa ushirikiano wa kimaendeleo ambapo kwa pamoja hubadilishana maarifa na kuelewa mafanikio makubwa na changamoto za kimaendeleo.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya mkutano huo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Dk Rahma Salum, alisema Zanzibar kama zilivyo nchi zingine duniani, inatekeleza mipango inayokwenda sambamba na mipango mikuu ya kidunia.

Zanzibar, alisema ilizindua dira ya mwaka 2020 - 2050 ambayo ndani yake mna malengo makuu ikiwamo uchumi wa bluu, usafiri na usafirishaji, utalii na huduma za kijamii, hivyo mkutano huo utajadili jinsi ya kuyatekeleza.

Alisema washirika wao wa maendeleo wanafuatilia kwa karibu kuona wanatekeleza mipango ya serikali na pia kuhakikisha wanatekeleza mipango ya kidunia na kutoachwa nyuma kwa malengo hayo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Bluu, Dk Aboud Suleiman Jumbe, alisema mkutano huo unatoa dira ya kuingia awamu mpya ya ushirikiano katika vipaumbele vya serikali vikiwamo afya, utawala bora, uvumilivu na ukuaji wa uchumi ambavyo UN ipo kusaidia vipaumbele hivyo.

# Waziri awasisitiza watu kunawa mikono

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wananchi kunawa mikono ipasavyo ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza.

Hayo aliyasema jana katika maadhimisho ya Siku ya Unawaji Mikono Duniani katika Ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni mjini Unguja.

Alisema unawaji wa mikono ni muhimu kwa jamii ili kujikinga na maradhi pamoja na kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

Waziri huyo alisema lengo kuu la maadhimisho hayo ni kuongeza uelewa kwa jamii juu ya unawaji mikono kwa ufanisi na kufuata hatua stahiki katika unawaji.

"Utaratibu maalumu wa kuosha mikono unafuata hatua maalumu, ambazo ni kutumia maji safi na salama yanayotiririka na sabuni kwa muda usiopungua sekunde ishirini," alisema.

Waziri Mazrui alisema utafiti unaonyesha unawaji mikono kwa maji safi ni hatua madhubuti za kuzuia magonjwa ya kuambukiza yakiwamo kipindupindu, kuharisha damu, maambukizi ya macho na maradhi ya mfumo wa kupumua.

Pia alisema wizara yake imetoa elimu katika shehia mbalimbali za Zanzibar kupitia vyombo vya habari, magari ya matangazo, masokoni na shuleni.

Waziri Mazrui aliwataka watendaji wa kitengo cha Kinga ya afya kuongeza bidii ya kuandaa vipindi maalumu vitakavyosaidia wananchi kujenga tabia ya kunawa mikono.

Mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Marko Musambazi, aliiomba Wizara ya Maji kuhakisha maeneo wanayoishi wananchi yanapata maji safi ili lengo la unawaji mikono litimie.

Alisema UNICEF iko tayari kushirikiana na Serikali ya Zanzibar kuhakikisha huduma za unawaji mikono zinapatikana katika skuli 121 katika wilaya tano ambazo zinahistoria kubwa za ugonjwa wa kipindupindu.




Mkuu wa Kitengo cha Mamlaka ya Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarak Hassan, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu bei elekezi ya nishati ya mafuta. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mamlaka sasa kutangaza bei elekezi ya gesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imesema inatarajia kutangaza bei elekezi ya gesi ya kupikia kama inavyotangaza nishati ya mafuta.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano cha ZURA, Mbarak Hassan, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za mamlaka hiyo, Maisara mjini Zanzibar.

Alisema bei hiyo elekezi kwa nishati hiyo ya gesi itasaidia kudhibiti upandishaji wa bei ya gesi holela

Alisema serikali ya Zanzibar inaendelea kufidia bei katika bidhaa zote za nishati ikiwamo ya mafuta ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wake.

Akitaja bei elekezi ya mafuta kwa mwezi Februari, alisema bei hiyo imeshuka ikilinganishwa na Januari, mwaka huu.

Mbarak alisema bei ya petroli ambayo imetangazwa kuanzia jana ni Sh. 2,298 tofauti ya Sh. 120 sawa na asilimia tano kutoka Sh. 2,418.

Kwa bei ya dizeli, alisema itauzwa kwa Sh. 2,345 tofauti ya Sh. 70 sawa na asilimia tatu kutoka Sh. 2,415 ya mwezi uliopita huku upande wa mafuta ya taa kwa mwezi huu yatauzwa kwa Sh. 1,890 tofauti ya Sh. 46 sawa na asilimia mbili ukilinganisha na bei ya Januari ambayo ilikuwa ikiuzwa kwa Sh. 1,936.

Alibainisha kwamba ZURA inapanga bei kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwamo kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kupitia bandari ya Dar es Salaam.

Alisema ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu. Jambo lingine, alisema ni kuangalia gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, kuangalia thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani, gharama za usafiri, bima na 'premium' hadi Zanzibar, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Aliwasisitiza wananchi kuwa bei hizo ndizo halali na kuwahimiza kununua mafuta katika vituo vilivyopo nchini na kudai risiti kila wanapopata huduma hiyo.

Kuhusu utoaji wa risiti za kielektroniki za VFMS katika vituo vya mafuta, alisema ZURA na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) watafanya kikao maalumu ili kuweka utaratibu katika masuala ya mafuta na gesi.

Sambamba na hayo, alibainisha kwamba lengo la mamlaka hiyo ni kuhakikisha huduma hiyo inaimarika zaidi na kuhahidi kwamba mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa wananchi katika mambo yote ya nishati.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**ANNA BALTAZAR MSEMWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne na result slip vyenye index namba **NS.1806/.0006** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **YUSUF MAKAMBA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DAR/BUG/RB/57311/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANZIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya KWIMBA**

**Kituo cha NYAMBITI Mkoa MWANZA**

**Usimamizi wa mirathi Na 01/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NDOMBELE TAMBILIJA KAYANDOGI WA LIGEMBE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MINZA SHADRACK LULU**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamzi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yeyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo walitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 02 Mwaka 2022 kabla huyo mwombajii hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 03 Mwezi 02 Mwaka 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro, Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi……12..2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY HABIBU EMILE WA KIHONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HALIMA ALLY EMILE.**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 15/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 08/02/2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RICHARD NARISISI MRISHO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NISSAN HOMMY** yenye namba za usajili **T 851 AVN** chasis namba **ARME24032063** engine namba **TD27035903A,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifan
**ARU/ARU/RB/49286/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**OMARY KASSIMU CHAMBI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.378 BQR aina ya SANLG.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichoponjirani yake
Taarifa ya polisi.
**NML/RB/75/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**
**Usimamizi wa Mirathi Na.01/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MASANJA NTEMI MWIGULU WA HINDUKI-MASWA.**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RICHARD SISI MASANJA.**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 Mwezi 03 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 04 Mwezi 02 Mwaka 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 534 YA 2021**

**PAPAA SOKOINE……………………………MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**VALERIAN FELIX CHUWA (Msimamizi wa mirathi ya marehemu Emmanuel Mleka Bulugu)…………..MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA VALERIAN FELIX CHUWA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 16/2/2022 mbele ya mwenyekiti E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 03 Mwezi February 2022.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE FABIAN NG'HOME** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 347 BDS – MAZDA.** ENGINE NO. **FS739639.** CHASIS NO. **LWEW110850.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PWA/MKU/RB/57617/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**

**Usimaizi wa mirathi Na 43/2018**

**Benjamini Kinyunyu…………………………….Marehemu**
**Ezekiel Benjamin Kinyunyu……………………Mwombaji**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI.**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jadala la mirathi.

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku tarehe 07 ya Mwezi March MWAKA 2022.
Imetolewa na Hakimu Mkazi leo siku ya tarehe 7 ya Mwezi Februari Mwaka 2022.

**HAKIMU MKAZI**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANGAZO

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA

*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 09 OF 2022

THE REPUBLIC

VERSUS

SOM PETROLEUM T) LIMITED……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Abdallah Hassan
Managing Director
SOM Petroleum (T) Limited
Pingo Area, Chalinze District Council
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of March, 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 3rd day of February, 2022.

……………………………………
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………………………

Signature……………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA

*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 01 OF 2022

THE REPUBLIC

VERSUS

QWIHAYA GENERAL ENTERPRISES CO. LIMITED……………………………………ACCUSED PERSON

To:

Jane Joseph Mbwambo, Leonard Igaga Mahenda and Benedicto Leonard Mahenda
Directors / Shareholders
Qwihaya General Enterprises (T) Limited
Zegereni Village, Kibaha District , Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 4th day of February 20 22

……………………………………
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………………………

Signature……………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF PWANI

*(AT PWANI)*

CRIMINAL CASE NO. 10 OF 2022

THE REPUBLIC

VERSUS

AISHA MTAULA……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Asha Mtaula
Plot No. 1, Block 4, Mbwewe Area,
Chalinze District Council , Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23rd day of February 20 22

……………………………………
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE

Served Upon Me/us:

Name……………………………………

Signature……………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA

*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 11 OF 2022

THE REPUBLIC

VERSUS

DAVIS MOSHA……………………………………ACCUSED PERSON

To:
Davis Mosha
Kwa Nelo Area, Chalinze Ward, Bagamoyo District
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 7th day of March 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 3rd day of February 20 22

……………………………………
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE

Served Upon Me/us:

Name……………………………………

Signature……………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………

# NKOMA AKOSHWA NA KASI, KIWANGO SIMBA QUEENS

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuendelea kupata ushindi katika kila mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini.

**Pongezi hizo za Nkoma zimekuja baada ya juzi timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Baobab Queens, katika mchezo wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.**

Huo ukiwa ni mchezo wa 10 mfululizo kwa Simba Queens kuibuka na ushindi kwenye ligi hiyo na kuendelea kuandika rekodi ya kutopoteza mechi yoyote msimu huu, hivyo kutesa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake wakiwa na alama 30 hadi sasa.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Nkoma alisema licha ya kupata ushindi huo anawapongeza wachezaji wake kupambana kwa kufuata maelekezo aliyowapa na kuendelea kukusanya pointi tatu zinazowafanya kujiimarisha kileleni.

"Mechi ilikuwa na ushindani mkubwa, Baobab Queens si wabaya, bali tulitumia madhaifu na ubora wao kuhakikisha tunapata pointi tatu na hilo tumefanikiwa na kuibuka na ushindi wa mabao 3-1," alisema Nkoma.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Baobab Queens, Miraji Fundi, alisema Simba walistahili kupata ushindi kwa sababu ya uzoefu na kutumia madhaifu ya mabaeki wake kupata mabao hayo.

Fundi alisema mechi ilikuwa nzuri, lakini kutokuwa na uzoefu ndio sababu ya wao kupoteza mchezo huo.

"Tumezidiwa kwa uzoefu, lakini safu yangu ya ulinzi haikuwa makini, Simba wanacheza kwa uzoefu mkubwa na wana timu nzuri, hivyo walistahili kupata ushindi.

"Tunaenda kufanyia kazi mapungufu yetu (hususan) safu ya ulinzi kwa ajili ya mchezo wetu ujao dhidi ya Fountain Gate, ili kuweza kupata pointi katika mchezo huo," alisema Fundi.

**SHUKRANI...**



Rais wa Rotary Club Bahari Tanzania, Diamond Carvalho (kulia), akimkabidhi cheti cha ushiriki, Mkurugenzi wa Wateja wa Kati wa Benki ya NBC, Moses Minja, wakati wa mashindano ya mchezo wa Gofu kwa ajili ya kukusanya fedha kwa kusaidia Shule ya Sekondari Mtakuja iliyoko Mbezi Beach, Dar es Salaam jana. Jumla ya Sh. milioni 44 zimekusanywa katika kampeni hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Watumishi kutinga uzi wa Geita Gold*

**Na Adam Fungamwangwo**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji Geita, Zuhura Michuzi, amewaagiza watumishi wote wa halmashauri hiyo makao makuu kuvaa jezi za timu ya Geita Gold kila Ijumaa nyakati za kazi wakiwa ofisini au wanapokwenda kukagua miradi, huku akitoa onyo kali kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na utengenezaji wa jezi feki za klabu hiyo.

Michuzi alisema hayo kwenye hafla ya utambulisho wa jezi mpya za timu hiyo, inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza.

"Ili kuenzi na kuisapoti timu yetu, ni kwamba nimeelekeza na kuagiza watumishi wote wa Halmashauri ya Mji Geita Makao Makuu kwamba, kila Ijumaa ni muhimu kuvaa jezi ya Geita Gold nyakati za kazi ofisini, au hata wanapokwenda kukagua miradi. Watakaokaidi tutasemezana nao vizuri tu kwa sababu timu hii ni ya kwetu sote," alisema Zuhura.

Mkurugenzi huyo pia alitoa onyo kwa wafanyabiashara watakaobainika kujihusisha na jezi feki za timu hiyo, akisema hatua kali zitachukuliwa juu yao.

"Tumepata kopi zaidi ya 3,000 za jezi kwa wachezaji na mashabiki na zimewekwa alama muhimu, zipo za aina tatu na za rika tofauti na tunatangaza vita kwa yeyote atakayeuza au kutengeneza jezi feki kuwa tutawachukulia hatua kali. Anayetaka kutengeneza na kukopi aje, tukae naye meza moja ya mazungumzo ili tuone wao watanufaikaje na sisi tutanufaika vipi kwa sababu hii ni biashara," alisema.

Geita Gold inashika nafasi ya nane ikiwa na pointi 17, kwa mechi 14 ilizocheza.

# Mlandege yaanika sababu ya vichapo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mlandege imesema kuanza vibaya katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar kumetokana na baadhi ya wachezaji kubweteka ikiwamo kutohudhuria mazoezini kama ilivyopangwa na kocha wa timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Mlandege, Jaala Abdallah Salum, alisema wachezaji wengi wanacheza kimazoea wakati ligi inaendelea katika ushindani mkubwa huku timu yao ikizidi kuwa chini.

Alisema miongoni mwa wachezaji ambao hawaudhurii mazoezini, wengi wao wanatoka katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Alisema suala la kubweteka wachezaji hao si tu kwa mzunguko huu wa pili, bali hata ule wa kwanza kulikuwa na tatizo hilo hivyo kusababisha timu kupoteza michezo mingi.

"Wachezaji hawatokei mazoezini, wanaokuja ni wachache mno, kinachosikitisha zaidi ni wale wa kikosi cha kwanza, sababu hii inachangia hata mwalimu kushindwa kufanya mipango yake vizuri," alisema.

Aidha alisema uongozi wa timu hiyo umechukua jitihada kadhaa katika dirisha dogo la usajili ikiwamo kuwaruhu wachezaji wanaotaka kuhama katika timu hiyo kwenda klabu zingine.

# TAHA hakuna kulala michuano Chalenji

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Mpira wa Mikono Tanzania (TAHA), umesema licha ya mashindano ya Kombe la Chalenji yaliyotarajiwa kufanyika nchini Ethiopia mwezi huu kusogezwa mbele, wao wanaendelea na maandalizi kuelekea michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Nicholous Mihayo, alisema awali, mashindano hayo yalipangwa kufanyika mwezi huu, lakini yakasogezwa mbele mpaka hapo tarehe mpya itakapopangwa tena.

"Mashindano hayo yalipangwa yafanyike mwezi huu, lakini yamesogezwa mbele mpaka ratiba itakapopangwa tena," alisema Mihayo.

Hata hivyo, alisema wakati huu wakiendelea kusubiri tarehe nyingine kupangwa, timu inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiweka sawa.

## ZISIKUPITE

### MANE KUONDOKA LIVER

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 29, atakuwa tayari kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto ikiwa Real Madrid au Barcelona watamnunua. (Goal)

### KANE AKUNWA NA CONTE

NAHODHA wa England, Harry Kane ana 'furahishwa sana' na kocha wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte. (Fabrizio Romano,via Express)

### ROMA WAMTAKA XHAKA

AS Roma inatarajia kufanya jaribio jipya la kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 29. (football.london)

### TIELEMANS ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kiungo wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24, ambaye thamani yake ni pauni milioni 40. (Star)

### EKITIKE AGOMBEWA

KLABU kadhaa za Ligi Kuu England zinamwania mshambuliaji wa Reims, Hugo Ekitike. Newcastle United ilishindwa kumsajili Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 19, katika dirisha dogo la usajili la Januari. (90 min)

### KEAN AWANIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Italia, Moise Kean katika majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, yupo kwa mkopo pale Juventus akitokea Everton. (Calciomercato,via Football Italia)

### KELLY KUTUA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inajiandaa kumnunua mlinzi wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 23, bila kujali kama watashuka daraja. (Football Insider)

### SPURS YAMTAKA VIDAL

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan na Chile, Arturo Vidal mwenye umri wa miaka 34. (La Latercera)

### FRAISL AWINDWA RANGERS

NORWICH City na Rangers wanamtazama mlinda mlango wa Schalke raia wa Austria, Martin Fraisl mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake utamalizika msimu wa majira ya joto. (Mail)

### MODRIC HADI MIAKA 40

KIUNGO wa kati wa Real Madrid na Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 36, amependekeza kwamba anaweza kuendelea kucheza hadi atakapofikisha umri wa miaka 40. (Marca).

### ASHLEY KUINUNUA DERBY

BILIONEA Mike Ashley bado anataka kuinunua klabu ya Championship, Derby County, lakini anatambua

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND SASA ATAJWA KUMRITHI MBAPPE PSG

**Tayari imeelezwa kwamba wawili hao hawatakuwa kwenye klabu zao za sasa wakati wa dirisha...**

**PARIS,** Ufaransa

STRAIKA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, atachukua nafasi ya Kylian Mbappe pale Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa gazeti la L'Equipe.

Mbappe na Haaland ndio wachezaji ambao wanatajwa zaidi sokoni kwa sasa na wanawaniwa na klabu kubwa barani Ulaya.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Haaland atatua PSG kuchukua nafasi ya Mbappe ambaye anatajwa atajiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu akiwa mchezaji huru.

**Wawili hao ambao kwa pamoja wamefunga mabao 43 kwenye mechi 50 kati yao msimu huu, wamekuwa lulu mno katika madirisha ya usajili barani Ulaya.**

Na sasa gazeti la L'Equipe limebainisha wazi kuwa, wawili hao hawatakuwa kwenye klabu zao za sasa wakati wa dirisha lijalo la usajili la majira ya joto.

Wakati PSG wakiwa wanaamini kuwa Mbappe atakwenda nchini Hispania kwa miamba Real Madrid, wanaona kwamba Haaland ndiye anayefaa kurithi mikoba yake.

Hata hivyo, PSG ambao ni miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, wanapambana kuhakikisha wanambakiza mchezaji huyo na kumshawishi kusaini mkataba mpya.

Na kama watashindwa kumbakiza mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, basi ndoano yao itatua kwa Haaland ambaye anawaniwa na miamba kama Madrid, Barcelona na timu kadhaa za Ligi Kuu England.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 918

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
LEICESTER
1 | 1.24
X | 6.63
2 | 10.04

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:

# KLOPP: SALAH FITI KUIVAA LEICESTER



**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah, yupo fiti kucheza dhidi ya Leicester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu England leo Alhamisi, kwa mujibu wa kocha Jurgen Klopp.

Salah ataingia kwenye mchezo huo ikiwa ni siku nne tu baada ya kutoka kupoteza fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), ambao walifungwa na Senegal ikiongozwa na mchezaji mwenza wa Liverpool, Sadio Mane.

Salah na Misri walipoteza fainali kwa mikwaju ya penalti ambapo nahodha huyo hakupiga penalti huko Cameroon.

Lakini Mane ambaye alipiga penalti ya ushindi, aliungana na Wasenegal katika mji mkuu Dakar siku ya Jumatatu kusherehekea ubingwa huo.

Mane hatakuwapo kwenye mchezo huo wa Liverpool wa leo kwa sababu bado yupo Senegal akiendelea kusherehekea ubingwa wa huo wa kwanza wa taifa hilo.

Klopp aliiambia LiverpoolFC.com: "Mo Salah sasa amerejea, nilizungumza naye tayari.

"Amesikitishwa sana bila shaka, lakini anaamini mambo yote yatakuwa sawa. Nilizungumza naye na kitu cha kwanza kabisa ambacho aliniambia, ilikuwa: 'Niko tayari.' Haha!

"Ni mchezaji mzoefu, kusema ukweli, kwa hiyo lazima tumuone, ni wazi atakuwa na muda kidogo na tutaona jinsi anavyojisikia."

# Ziyech atundika daluga Morocco



**LONDON,** England

KIUNGO wa Chelsea, Hakim Ziyech, ameamua kustaafu kuichezea timu ya Taifa ya Morocco, kutokana na mgogoro wake na kocha mkuu wa timu hiyo.

Nyota huyo wa zamani wa Ajax, Ziyech hajaichezea nchi yake tangu kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Burkina Faso Julai mwaka jana baada ya kugombana na kocha, Vahid Halilhodzic.

Ziyech hakujumuishwa katika kikosi cha Morocco kwenye michuano ya mataifa ya Afrika iliyomalizika hivi karibuni.

Bila yeye, Morocco ilitinga robo fainali, lakini ilitolewa na Misri ambayo imemaliza ikiwa nafasi ya pili baada ya kufungwa kwenye fainali na Senegal.

Baada ya Morocco kuondolewa kwenye mashindano hayo, Halilhodzic alisema kwamba, Ziyech hatakaribishwa tena kwenye kikosi hicho "hata kama jina lake lingekuwa ni Lionel Messi".

Ziyech, akizungumza na ADSports TV, alisema anaamini muda wake umefika na anaamua kukaa pembeni na hataichezea tena Morocco kwa kipindi ambacho Halilhodzic ataendelea kuwa kocha wa timu hiyo.

"Nawaelewa, lakini sitarudi kwenye timu ya Taifa ya Morocco na huu ni uamuzi wangu wa mwisho," alisema Ziyech mwenye umri wa miaka 28.

"Ni wazi kwamba mambo kwa upande wangu hivi sasa hayako sawa, akili yangu ni kuendelea kufanya kile ninachofanya na klabu yangu."

## HABARI MICHEZO


# ,137,180

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/02/21 | 18:00 | Brentford vs Crystal Palace | 2.60 | 3.09 | 2.84 |
| 02. 12/02/21 | 18:00 | Peterborough vs Preston | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 03. 12/02/21 | 18:00 | Reading vs Coventry | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 04. 12/02/21 | 18:00 | Birmingham vs Luton Town | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 12/02/21 | 18:00 | Nottingham vs Stoke City | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 06. 12/02/21 | 18:15 | Villarreal vs Real Madrid | 2.74 | 3.32 | 2.54 |
| 07. 12/02/216 | 18:15 | Perugia vs Frosinone | 2.40 | 3.14 | 2.90 |
| 08. 12/02/21 | 20:00 | Napoli vs Inter | 2.81 | 3.41 | 2.44 |
| 09. 13/02/21 | 15:00 | Sheffield Wed vs Rotherham | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 10. 13/02/21 | 16:00 | Alaves vs Valencia | 3.04 | 3.24 | 2.36 |
| 11. 13/02/21 | 18:00 | Real Oviedo vs Huesca | 2.46 | 3.15 | 2.81 |
| 12. 13/02/21 | 19:00 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.61 | 3.30 | 2.56 |
| 13. 13/02/21 | 19:30 | Leicester vs West Ham | 2.85 | 3.45 | 2.38 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 10/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 1673 | Arema vs Persiraja Banda | 1.13 | 6.37 | 17.37 |
| 16:00 | 2428 | Addis Ababa City FC vs Ethiopia Bunna SC | 3.04 | 2.94 | 2.32 |
| 16:00 | 2563 | Police FC (UGA) vs FC Saints | 2.15 | 3.23 | 3.08 |
| 16:30 | 2149 | Al Sharjah SC vs Al Dhafra | 1.35 | 4.85 | 6.59 |
| 16:40 | 1993 | Al-Sailiya SC vs Al Rayyan SC | 3.86 | 3.57 | 1.78 |
| 16:45 | 5397 | Persela Lamongan vs Persebaya Surabaya | 4.43 | 3.52 | 1.70 |
| 17:00 | 2574 | Sliema Wand vs Vittoriosa Stars | 1.45 | 4.61 | 5.18 |
| 17:00 | 3123 | Jamshedpur vs Kerala Blasters FC | 2.08 | 3.33 | 3.13 |
| 17:00 | 5069 | Islami Qalqilya vs Jabal EL Mokaber | 6.00 | 4.16 | 1.44 |
| 17:00 | 5727 | Vitoria Guimaraes U23 vs FC Famalicao U23 | 2.29 | 3.27 | 2.79 |
| 17:30 | 1395 | Alanyaspor vs Adana Demirspor | 2.22 | 3.28 | 2.90 |
| 18:00 | 2159 | East Riffa vs Riffa Club | 4.04 | 3.47 | 1.77 |
| 18:00 | 3440 | Apollon Limassol vs AEL Limassol | 1.78 | 3.60 | 4.35 |
| 18:00 | 4931 | U Craiova SA vs Botosani | 3.05 | 3.00 | 2.39 |
| 18:15 | 3228 | Atromitos vs Lamia | 2.08 | 3.06 | 3.75 |
| 18:30 | 3586 | National Bank vs Smouha Club | 2.88 | 2.88 | 2.63 |
| 18:50 | 3619 | Al Arabi Doha SC vs Al Ahli Doha SC | 1.61 | 4.14 | 4.23 |
| 18:50 | 4553 | Al Khoor vs Al Gharafa SC | 4.25 | 3.96 | 1.63 |
| 19:00 | 4369 | Bahir Dar Kenema FC vs Hawassa Kenema SC | 3.09 | 2.89 | 2.32 |
| 19:30 | 3934 | JS Kabylie vs MC Alger | 1.85 | 3.19 | 4.05 |
| 20:00 | 1439 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs AS Tel Aviv University W | 1.99 | 4.30 | 3.05 |
| 20:00 | 3379 | Anorthosis Famagusta vs Aris Limassol | 1.81 | 3.56 | 4.25 |
| 20:00 | 4071 | Thagafi Tulkarem vs Shabab AL Khaleel | 5.59 | 4.05 | 1.48 |
| 20:00 | 5393 | Atalanta vs Fiorentina | 1.75 | 3.90 | 4.05 |
| 20:30 | 1262 | Besiktas vs Goeztepe | 1.48 | 4.15 | 5.40 |
| 20:30 | 5812 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 2.29 | 3.87 | 2.47 |
| 20:30 | 5856 | FC Thun vs FC Lugano | 2.66 | 3.43 | 2.32 |
| 20:45 | 1153 | Hapoel Raanana W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 3.32 | 4.13 | 1.80 |
| 20:55 | 4044 | Dinamo Bucuresti vs Universitatea Craiova | 5.29 | 3.67 | 1.62 |
| 21:00 | 2834 | GD Chaves vs Rio Ave | 2.45 | 3.08 | 2.84 |
| 21:00 | 4539 | Birkirkara vs Fgura United | 1.16 | 7.13 | 10.59 |
| 21:00 | 5379 | Ismaily SC vs Coca Cola | 2.38 | 2.77 | 3.41 |
| 21:00 | 5951 | NEC Nijmegen vs GO Ahead Eagles | 1.88 | 3.33 | 3.72 |
| 21:30 | 2899 | Nova Iguacu RJ vs Boavista RJ | 2.33 | 2.89 | 3.08 |
| 21:30 | 5059 | SE Santa Maria DF vs Gama DF | 4.15 | 3.96 | 1.65 |
| 22:00 | 5107 | EC Prospera SC vs GE Juventus SC | 3.15 | 2.80 | 2.55 |
| 22:40 | 2971 | Glasgow City W vs Celtic W | 2.09 | 3.62 | 2.90 |
| 22:45 | 5433 | Wolverhampton vs Arsenal | 3.40 | 3.11 | 2.25 |
| 22:45 | 5592 | Liverpool vs Leicester | 1.24 | 6.63 | 10.04 |
| 23:00 | 2258 | Orsomarso vs Llaneros FC | 2.75 | 2.90 | 2.56 |
| 23:00 | 3096 | Juventus vs Sassuolo | 1.51 | 4.28 | 5.58 |
| 23:00 | 3866 | Nantes vs Bastia | 1.56 | 3.84 | 5.71 |
| 23:30 | 5078 | Athletic Bilbao vs Valencia | 1.82 | 3.45 | 4.24 |

### IJUMAA - 11/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:30 | 1311 | Azuniz FC vs CE Uniao PR | 1.64 | 3.54 | 4.84 |
| 01:00 | 1354 | Santos vs SAO Bernardo FC SP | 1.44 | 3.85 | 6.74 |





# TFF YAWAITA WAAMUZI LIGI KUU BARA HARAKA

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja tu baada ya Klabu ya Yanga kulalamika juu ya kile walichodai mwenendo usioridhisha wa waamuzi, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limetangaza kuitisha semina ya siku tatu ya waamuzi wa Ligi Kuu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TFF kwa vyombo vya habari na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa litafanya semina hiyo kuanzia Februari 15, mwaka huu na lengo ni kutazama na kupitia changamoto, ikiwamo kuboresha maeneo mbalimbali.

"Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), litafanya semina ya siku tatu kwa waamuzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia Februari 15, mwaka huu.

"Huu ni utaratibu wa kawaida kufanya semina kwa waamuzi kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu. Semina hiyo itahusisha waamuzi wote wa Ligi Kuu pamoja na Kamati ya Waamuzi," ilieleza taarifa hiyo.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya TFF, Nassor Hamduni, alisema semina hiyo haihusiani na tamko la Yanga, badala yake ni utaratibu wa kawaida wa shirikisho hilo kupitia kamati hiyo.

"Ni utaratibu wa kawaida kila nusu ya msimu wa ligi, nia kutathmini ili kuona kama kuna kasoro zirekebishwe," alisema mwenyekiti huyo.

Kuhusu tamko la Yanga, alisema kuwa anachojua hayakuwa malalamiko, kama walivyosema wenyewe bali ni kukumbusha, huku akikataa kuwa baadhi ya waamuzi wanaboronga kwenye mechi za Ligi Kuu.

"Mimi sioni kama wanaboronga, wanachezesha kwa haki, ila kwenye semina yetu tutakumbushana yale mazuri ili tuendeleze na yale mapungufu tuyarekebishe," alisema mwamuzi huyo wa zamani wa kimataifa.

# Klabu 9 ndani mashindano ya kuogelea ya Taliss

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya klabu tisa zimethibitisha kushiriki katika mashindano ya Kuogelea ya Taliss-IST yaliyopangwa kufanyika Februari 26-27, mwaka huu kwenye Bwawa la Kuogelea la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) Masaki.

Meneja wa Klabu ya Taliss-IST, Hadija Shebe, amezitaja klabu hizo kuwa ni Moshi, Wahoo (Zanzibar), FK Blue Marlins (Dar es Salaam), Dar es Salaam Swimming Club (Dar es Salaam), Bluefins (Dar es Salaam) na Mwanza Swimming Club.

Pia katika orodha hiyo, kuna Klabu ya Mis Piranhas (Morogoro), Champions Rise (Dar es Salaam) na wenyeji wa mashindani hayo, Taliss-IST.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Hadija alisema maandalizi ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na waogeleaji wanafanya mazoezi ili kushindania zawadi mbalimbali siku hiyo.

Alisema waogeleaji zaidi ya 200 wanatarajia kushiriki katika mashindano hayo yaliyodhaminiwa na Jubilee Insurance, Azam, Pepsi, Auric Air, Dolphin Tours and Safari limited, Burger 53 na Knight Support.



Agustino Lucas, akishindana katika mashindano yaliyopita ya kuogelea. **PICHA: MAKTABA**

Hadija alisema waogeleaji watashindana katika umri tofauti katika staili mbalimbali kwa mujibu wa taratibu, lakini kutakuwa na kundi la waogeleaji chini ya miaka nane, tisa, 10, 11 na 12, 13 na 14, na zaidi ya miaka 15.

Alisema mbali ya staili tano za kuogelea, waogeleaji hao watashindana katika 'relei' kwa mtindo wa 'Individual Medley (IM) na Freestyle'. Kwenye IM, waogeleaji watachanganya staili nne ambazo ni butterfly, backstroke, breaststroke, na freestyle.

"Waogeleaji watakaoshinda katika mashindano hayo watazawadiwa medali na vikombe, tunawaomba wadhamini waendelee kujitokeza ili kufanikisha mashindano haya ambayo ni maarufu na yenye mvuto mkubwa," alisema Hadija.

# Michezo

Alhamisi Februari 10, 2022

Nipashe




## Klopp: Salah fiti kuivaa Leicester leo

NI USHINDI TU...



Rais wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed "Mo" Dewji (kulia), akiteta jambo na Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Pablo Franco, baada ya kumaliza kuzungumza na wachezaji wa timu hiyo kuelekea mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yaipigia hesabu Biashara

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wamerejea kambini kujiandaa kutafuta ushindi dhidi ya Biashara United, katika mchezo wa hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini Dar es Salaam, Nabi alisema hakuna mechi iliyo rahisi na anaamini kila mchezo kwao ni fainali na kuwataka wachezaji kuwa makini kwa kucheza kwa ushirikiano mkubwa ili kupata matokeo chanya.

Alisema anatambua ndani ya kikosi chake hakuna mchezaji staa na kila mmoja anatakiwa kupambania timu kuhakikisha wanapata matokeo mazuri hususani katika mechi iliyoko mbele yao ambayo wakipoteza wanatoka katika michuano hiyo.

"Hii si ligi ambayo ukipoteza utakuwa bado unaendelea, ni mchezo wa mtoano na timu inayofanikiwa kusonga mbele inawakilisha nchini katika michuano ya kimataifa, kwa hatua hii tunatakiwa kupigania na kupata ushindi," alisema Nabi.

Alisema wanaendelea kufanyia kazi madhaifu yao kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kusonga mbele katika michuano hiyo kwa kuibuka na ushindi mbele ya Biashara United. Yanga itakuwa mwenyeji wa mchezo huo dhidi ya Biashara United katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumanne ijayo.

# PABLO AISHTUKIA ASEC, AISOMA, AIONYA SIMBA

**Na Saada Akida**

●●●Atabiri mechi ngumu, Mo Dewji awaweka kikao wachezaji, Wawa asema anaijua, awatoa hofu mashabiki, lakini...

WAKATI wakiendelea na maandalizi ya mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, itakayopigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema amewasoma wapinzani wao hao na kubaini ni timu bora, hivyo hautakuwa mchezo rahisi, lakini wanajipanga kusaka pointi tatu nyumbani.

Huo ni mchezo wa kwanza katika hatua ya makundi, na baada ya mechi hiyo, Simba itaifuata USGN ya Niger Februari 20, mwaka huu kabla ya wiki moja baadaye kwenda kukipiga na RS Berkane ya Morocco.

Asec Mimosas kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Ivory Coast ikiwa imeshinda mechi zake zote saba iliyocheza hadi sasa katika ligi hiyo inayojumuisha timu 14, ikifuatiwa na Gagnoa yenye pointi 19 baada ya michezo nane huku San-Pedro ambayo nayo imeshuka dimbani mara nane, ipo nafasi ya tatu na alama zake 14.

Akizungumza na gazeti hili juzi katika Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, Pablo alisema amepata taarifa za wapinzani wao na kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake hasa kwa kuwapa mazoezi maalumu safu yake ya ushambuliaji.

Alisema baada ya kumalizika kwa mchezo wa ligi dhidi ya Mbeya Kwanza, alitoa mapumziko ya siku moja kwa wachezaji wake na tayari tangu juzi walirejea kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo dhidi ya Asec Mimosas.

"Baada ya ratiba ngumu kwa wiki iliyoisha, tunapata muda wa kufanya mazoezi ya kutosha na kuwapa mbinu za kufunga mabao washambuliaji wangu kwa sababu tumekuwa tukitengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

"Tunafanyia kazi kila nafasi ikiwamo safu ya ulinzi, kiungo, winga na kuweka umakini sana kwa washambuliaji kwa sababu mechi zilizopita tumetengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia," alisema Pablo.

Alisema ameandaa programu maalum kwa kila nafasi kuelekea mchezo huo wa Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuhakikisha wanafanya vizuri na kupata ushindi katika uwanja wa nyumbani.

> **"Tumepata taarifa za wapinzani wetu, tumeanza kufanyia kazi ubora wao, lakini madhaifu yao, ili kuhakikisha tunapata ushindi na pointi tatu za nyumbani," alisema Pablo.**

Kuhusu wachezaji majeruhi, alisema Taddeo Lwanga anaendelea vizuri na jana Denis Kibu alianza mazoezi mepesi baada ya kupata majeraha na kukosa mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa upande wa beki wa kati wa Simba, Pascal Wawa, alisema utakuwa mchezo mgumu kwa kuwa Asec Mimosas ni timu nzuri, lakini wao kama wachezaji wanafahamu umuhimu wa mchezo huo.

"Tunajua mchezo utakuwa mgumu kutokana na ubora wa Asec na historia yao Afrika, lakini tumejipanga hatutaingia uwanjani kwa presha wala kucheza kwa woga," alisema Wawa ambaye ni raia wa Ivory Coast.Naye beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, alisema walikuwa na mipango ya kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, lakini baada ya kushindikana sasa wamehamishia nguvu zote kwenye Kombe la Shirikisho.

"Mwanzoni tulitaka nafasi za juu katika Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini baada ya kushindikana tumehamishia nguvu Shirikisho, tunataka malengo tuliyokuwa nayo tuyakamilishe na kuhakikisha tunaanza kwa ushindi dhidi ya Asec Mimosas," alisema Kapombe na kuongeza;

"Wachezaji tumejipanga kuhakikisha tunawapa furaha mashabiki wetu kwa kufanya vizuri katika michuano hii, tunawaheshimu Asec Mimosas ni timu bora tunaifuatilia inaongoza ligi ya kwao, lakini tumejipanga kukabiliana nao na hatimaye tubakishe pointi nyumbani," alisema Kapombe.

Katika hatua nyingine, Rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji, jana alikutana na kufanya mazungumzo ya mambo mbalimbali na wachezaji pamoja na benchi la ufundi katika kikao maalum kilichofanyika jijini Dar es Salaam kuelekea mechi hiyo.

9 770856 541002 >